Soma Neno la Mungu

Ndoa

Mambo muhimu unayo takiwa uyafanye ili upate kuilinda na kuiponya ndoa yako

Sehemu ya Kwanza

***Tahadhari**: Kitabu hiki ni kwa ajili ya watu wazima tu!*

Na; Mwl.
Mr. & Mrs. Stephen Mwakatwila

Simu: +255 (0)75 484 9924 | E-mail: steven@mwakatwila.org | Tovuti: www.mwakatwila.org

UTANGULIZI

Bwana Yesu Kristo apewe sifa sana. Mimi na familia yangu tunawasalimu katika jina la Yesu Kristo aliye hai. Mimi na familia yangu hatujambo kabisa. Tunamshukuru Mungu aliyetuokoa na kutupigania. Tunamshukuru Mungu ambaye ametupa somo hili lenye kichwa

"MAMBO MUHIMU UNAYO TAKIWA UYAFANYE ILI UPATE KUILINDA NA KUIPONYA NDOA YAKO"

Ni somo la ndoa lakini kila mtu mwenye akili timamu aliyeoa au kuolewa au ambaye anatarajia kuoa au kuolewa hivi karibuni, anaweza kujifunza. Mwombe Roho Mtakatifu akufundishe kile alicho kikusudia kukufundisha. Ninakukaribisha karibu tuanze kujifunza. Hebu yasikie maneno haya ya Bwana yasemavyo;

"Bwana mkombozi wako, mtakatifu wa Israeli, asema hivi; mimi ni Bwana, Mungu wako, nikufundishaye ili upate faida, nikuongozaye kwa njia ikupasayo kuifuata." (Isaya 48:17)

Mpango wa Mungu katika somo hili ni wa kukupa wewe faida. Hebu mnyenyekee Mungu katika ujumbe huu na ninakuakikishia kweli, utapata faida baada ya kujifunza kila kitu kilichomo ndani ya somo hili. Mungu akubariki sana karibu tujifunze

MATATIZO MAKUBWA

Siku moja nilikuwa nimepata mwaliko kutoka kwa Askofu mmoja. Alinialika niende pamoja naye kwenye Shughuli za kuwa weka wakfu watumishi wa Mungu katika huduma ya uchungaji. Nilimkubalia kwani nilipata kibali kutoka kwa Bwana kwenda huko, sehemu hiyo ilikuwa mbali sana na sehemu ninayoishi, ilinilazimu kulala huko huko kwa usiku mmoja. Baada ya shughuli zile, usiku nilipokuwa nataka kulala tu, Roho Mtakatifu aliniambia maneno haya "Steven nataka nikufundishe somo la ndoa". Nikalipokea neno hilo moyoni mwangu, baada ya kulipokea neno hilo, nipata maswali mengi sana, nilijiuliza je! Ndoa yangu ina matatizo? Sijui kuishi vema na mke wangu? nk. Nilipokuwa katika kujiuliza sana maswali hayo, Roho Mtakatifu akasema nami tena, akaniambia somo hilo ni kwa ajili ya watu wote. Unajua Mungu anapokuambia watu wote ni tofauti sana na anapokuambia ni kwa ajili ya watoto wangu. Sasa nikatambua kuwa somo hili ambalo Bwana amekusudia kulifundisha ni kwa ajili ya watu wote, yaani watoto wa Mungu na watu wake wote. Niliporudi kutoka safari ile nikamshirikisha mke wangu kitu hicho alichoniambia Bwana, tukaanza kuomba ili Bwana atufundishe kama alivyokusudia, nikakaa mkao wa kujifunza.

Jambo la kwanza kabisa ambalo Bwana alianza kunifundisha alianzia kunionyesha namna watu wake walivyo na matatizo mengi, wawe waliookoka, wasiokoka, watumishi wake, viongozi wa serikali nk. Alianza kwa kuniwekea kitu hicho, nilianza kuona kila tulipokwenda sehemu mbalimbali kwenye huduma za kufundisha semina ziwe siku za nyuma na hata wakati huu, tunakutana na watu wengi wakiwa na matatizo mengi sana. Watu wengi wanatufuata wakihitaji maombi na hata wengine kutupigia simu na kutuandikia jumbe nyingi sana kwa kutumia simu, barua kwa njia ya mtandao wa internet wakiomba ushauri au maombi. Tulipoanza kuyaangalia hayo matatizo yao tukagundua kuwa katika asilimia mia moja ya hayo matatizo asilimia themanini ni matatizo yanayotokana na magomvi katika ndoa zao. Baada ya kujifunza hapo, ndipo tulipoweka bidii ya kujifunza hicho Bwana anachotaka kutufundisha. Ndoa nyingi sana hazipo vizuri, na kwa kuwa hazipo vizuri imepelekea maumivu makali sana kwa hao wana ndoa. Ukifuatilia kwa makini utagundua kuwa, watu wengi sana wanaoumwa leo hii au walio na matatizo ya kiuchumi au watu wanaokufa mapema, chanzo chake ni magumu yaliyomo ndani ya ndoa.

Angalia leo hii matatizo yanayotokea kwa watoto wengi ya kukosa maadili na hata uwezo mdogo darasani, unajua tatizo ni nini? Ni matatizo yalimo ndani ya ndoa zao! Hata leo hii ukifuatilia watu wengi sana ambao Mungu amewaita kwenye utumishi wake, wamekwama, kisa kikubwa kilichowakwamisha ni tatizo lililomo kwenye ndoa yao. Unajua matatizo yanayotokea kwenye ndoa yanapelekea watu wengi kukosa kuupata uzima wa milele, kwa sababu tu hawakukaa vizuri katika ndoa zao. Ukiangalia watu wengi sana wana matatizo kwenye eneo la kupokea majibu ya maombi yao. Tulipotulia tukagundua tatizo linalopelekea washindwe kupokea majibu yao chanzo chake ni

kutokana na tatizo lililopo kwenye ndoa yao. Baada ya kuyaona hayo tukapata hamu ya kuanza kujifunza kwa bidii kile ambacho Mungu anataka kutufundisha ili tuwafundishe watu wake. Fahamu neno la Mungu linasema hivi;

"Bwana, mkombozi wako, mtakatifu wa Israeli, asema hivi; mimi ni Bwana, Mungu wako, nikufundishaye ili upate faida, nikuongozaye kwa njia ikupasayo kuifuata."
(Isaya 48: 17)

Mungu anataka upate faida katika kila jambo au kwa maana nzuri anataka ufanikiwe. Ili upate mafanikio anachofanya anakuletea mafundisho au maagizo maalumu.

UHABA WA SOMO LA NDOA

Jambo la pili ambalo Bwana alitufundisha ambalo ndilo linalopelekea leo hii kuwe na matatizo kwenye ndoa nyingi ni hili la watu kukosa ufahamu wa ni nini kiwapasacho kufanya waingiapo kuishi katika maisha ya ndoa. Ukiangalia utagundua kuwa somo la ndoa ni haba kanisani. Wewe angalia mwaka jana umesikia somo kama hilo hapo kanisani kwenu? Au mwaka huu kuna semina ya ndoa imepita hapo kanisani kwenu? Unajua hata zipitapo ona maandalizi yake yalivyo bubu. Leo hii ni rahisi kuwalaumu watu kuwa hawaishi maisha mema katika ndoa zao bila ya kuangalia chanzo cha matatizo ni nini. Ngoja nikuulize swali. Kabla haujaoa au kuolewa ulipokea mafundisho kutoka kwa mchungaji wako akikufundisha mambo muhimu unayotakiwa uyafanye utakapo anza kuishi na huyo mumeo au mkeo? Na kama alikufundisha je! Alikufundisha kwa undani kabisa? Au ndio juu-juu tu? Wewe jijibu mwenyewe, utaona wengi hawana elimu ya namna hiyo, naizungumzia elimu ya Kibiblia, si ile ya kumuona mama anavyoishi na baba au baba anavyoishi na mama au kaka anavyoishi na mke wake. Somo la ndoa kanisani limekua siri. Hilo ndilo tatizo kubwa, angalia utagundua kuwa watu wengi wanaanza kujifunza kuishi maisha mema ya ndoa wakiwa ndani ya ndoa, fikiri wameanza kujifunza wakiwa na miaka kumi au ishirini kwenye hiyo ndoa, swali langu kwa nini wasianze kujifunza somo hilo kabla ya kuingia ndani ya ndoa?

Ninavyosema somo la ndoa, unaweza kuwaza habari za tendo la ndoa, sikia, maisha ya ndoa ni zaidi ya tendo la ndoa! Kuna mambo mengi ambayo wanandoa wanapaswa wajifunze kuliko hilo moja tu, ambalo ndilo siri. Mungu alianza kwa kutufundisha hayo. Alinifundisha kuwa kila mtu ambaye ana akili timamu anapaswa kujifunza SOMO LA NDOA au habari za kuishi na mke au mume kwa upana awe ndani ya ndoa au akitarajia siku moja kuoa ama kuolewa. Fikiri leo hii watu wanaanza kujifunza wakiwa tayari ndani ya ndoa, wakiwa na watoto tayari nk. Unajua watu wa jinsi hiyo ni vigumu sana kupokea kitu kipya, wewe ona leo hii, kama kuna semina ya ndoa, utaona wanaokimbilia ni kina mama, unajua ni kwa nini? Wanaume wengi, wanajiona wanajua kwa kuwa wameoa na wamepata watoto, sasa unapomwambia kuna somo la ndoa hawaoni umuhimu wake. Ngoja nikupe mfano, unawafahamu madereva wa magari? Kila dereva anajiona

yeye ni bora kuliko mwenzake, sasa ukimwita dereva eti umfundishe kuendesha gari wakati yeye anajiona anajua ni ngumu sana kukuelewa. Ndivyo ilivyo hata leo kwa watu wengi sana ni shida kuitikia wito wa kuja kujifunza somo hili la ndoa. Hebu sisi tuanze kujifunza.

SI MPANGO WA MUNGU NDOA IWE SEHEMU YA MATATIZO

Ukiziangalia ndoa nyingi utaona wazi kuwa ndoa hizo zipo kwenye taabu sana. Wana ndoa wengi baada ya kuanza kuishi kama mke na mume wamejikuta wameangukia kwenye magomvi yanayopelekea maumivu makubwa. Na wengi wamefikiri au wamepokea na kuamini kuwa hayo ndiyo maisha ya ndoa. Watu wengi wanafikiri hivyo, Wewe sikiliza mahubiri au nasaha za wazazi siku ya sherehe ya ndoa. Utasikia muhubiri akisisitiza sana habari za kuvumiliana. Hata wazazi wa hao wanandoa utawasikiliza wakisema sana habari hizo za kuvumiliana, kwa nini kuvumiliana? Kama si kutuambia kuwa huko ndani ya ndoa kuna matatizo? Huwezi kusema vumilia kama hakuna teso, kwa kuwa ndoa nyingi sana zimekuwa na mateso ni rahisi kuona na kukubali kuwa ndoa ni sehemu ya mateso. nakumbuka miaka ile ya nyuma kabla sijaoa tulikuwa na msemo mmoja tukiona kijana mwenzetu anaoa, tulisema "Jamaa ananunua matatizo". Unajua ni kwanini tulikuwa na msemo huo? Tuliona ndio mfumo wa ndoa nyingi zilivyo. Mimi baba yangu alikuwa askari, bahati nzuri baba alikuwa afisa mkubwa tu. Kesi nyingi ziliamuliwa hapo nyumbani, hasa za masuluhisho ya ndoa. Niliona namna kina mama wanavyopigwa na waume zao na hata wanaume wanaopigwa na wake zao, palipo na watu wengi kuna mambo mengi sana! Ilikua ni kitu cha kawaida kusikia fulani amemtandika mke wake na kesho tukamuona huyo mama akiwa amevimba kweli usoni. Tuliona kuwa hayo ndiyo maisha ya ndoa, niliona namna watu wanavyofukuza wake zao na kuoa wengine; hiyo ilikuwa ni jambo la kawaida kabisa.

Tulijenga mawazo kama hayo kuwa maisha ya ndoa ni ya matatizo tu, naamini hata watu wengi wanafikiri hivyo, wamepokea hivyo, ndio maana kila anayeoa au kuolewa lazima aambiwe kuwa kavumilie. Sijui wewe uliambiwaje? Watu wengi wanatiana moyo utasikia wakisema, "jipe moyo mpendwa hilo ndilo jaribu lako". Utafikiri kweli Mungu ndio kalipanga hilo jaribu, sikiliza, si mpango wa Mungu ndoa iwe sehemu ya mateso au iwe ni sehemu ya matatizo yanayopelekea watu kukosa amani na hata kupata magonjwa na kufa au kushindwa kumtumikia Mungu wao.

MUNGU ANACHUKIA AONAPO MATATATIZO KATIKA NDOA

Hebu uangalie moyo wa Mungu ulivyo, anasema .

"Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema Bwana, ni mawazo ya amani, wala si mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho" (YEREMIA 29:11)

Fikiria hayo ndani ya moyo wako, Mungu hajawahi kukuwazia wewe mabaya, anakuwazia amani na matumaini au mafanikio, kama hajawahi kukuwazia mabaya, basi hata hilo tatizo kwenye ndoa yako yeye hajawahi kuliwazia likutokee. Anaiwazia amani na mambo mema na utulivu katika hiyo ndoa yako. Ukiona magumu katika ndoa yako fahamu chanzo chake ni adui shetani, unajua ni kwanini nasema hivyo? Ni kwa sababu Mungu anaiheshimu sana ndoa yako. Tazama maneno haya yasemavyo;

"Ndoa na iheshimiwe na watu wote..." (EBR13:4).

Mungu amemwagiza kila mtu aiheshimu ndoa. Iwe yake au ya mtu mwingine. Hilo ni agizo mojawapo ambalo kila mtu amepewa haijalishi ni mtumishi wa Mungu, baba au mama, wifi, shangazi au mjomba , mkuu wako wa kazini nk.

Mungu asingelituagiza sisi watu wake tuziheshimu ndoa zetu kama yeye haziheshimu hizo ndoa. Mungu anaziheshimu ndoa zetu sana. Nataka nikuulize swali je! Wewe unaiheshimu ndoa yako? Au ya watoto wako? Au ya jirani yako? Au ya ndugu yako? Au ndoa ya hao wamwaminio Mungu hapo kanisani? Watu wengi hapo wamekwama. Wengi hawaziheshimu ndoa zao au za watu wengine. Tazama mfano huu utaelewa, Kuhani Haruni mtumishi wa Mungu yeye na dada yake aitwaye Miriamu, hawakuiheshimu ndoa ya ndugu yao Musa. Mungu aliwakasirikia sana; Tazama maneno haya.

"Kisha Miriamu na Haruni wakamnenea Musa kwa sababu ya mwanamke Mkushi aliyekuwa amemwoa; maana alikuwa amemwoa mwanamke Mkushi..... Hasira za Bwana zikawaka juu yao; naye akaenda zake. Kisha hilo wingu likaondoka kutoka pale juu ya hema; tazama, Miriamu akawa mwenye ukoma, mweupe kama theluji; Haruni akamwangalia Miriamu, na tazama, yu mwenye ukoma kisha haruni akamwambia Musa, Ee bwana wangu, nakusihi sana usituwekee dhambi juu yetu, kwa kuwa tumefanya ya upumbavu, na kufanya dhambi. Nakusihi, asiwe kama mmoja aliyekufa, ambaye nyama ya mwili wake nusu imelika, hapo atokapo tumbo la mama yake. Musa akamlingana Bwana, akasema, mpoze, Ee Mungu, nakusihi sana. Bwana akamwambia Musa, je! Kama baba yake angalimtemea mate usoni tu, hangaliona aibu muda wa siku saba? Na afungwe nje ya kambi muda wa siku saba, kisha baada ya hayo ataletwa ndani tena." (Hesabu 12: 1-14)

Ona anasema habari za baba kumtemea mate mwanawe, unajua maana yake nini? ni kumlaani au kumwona kama kinyaa vile, au kumdharau kabisa. Mungu alimtemea mate Miriamu usoni kisa hakuiheshimu ndoa ya Musa. Kilichomsaidia Haruni kilikuwa ni ule ukuhani aliokuwa nao, siku alipostaafu tu, neno linasema alipovua vazi la kikuhani tu, alidodoka akafa. Mnisikilize watumishi wote wa Mungu. Heshimuni ndoa za watu, kwani Miriamu alikua ni Nabii;

"Na Miriamu, nabii mke, ndugu yake Haruni....." *(Kutoka 15:20)*

Mungu alimpiga kwa ukoma kisa, hakuiheshimu ndoa ya mtu. Hebu fikiri uone jinsi Mungu anavyo heshimu ndoa, alikuwa tayari kumpiga nabii Miriamu kwa ukoma kwa sababu hakuiheshimu ndoa ya kaka yake, kumbuka Haruni, Musa, na Miriamu hawa ni ndugu kabisa. Leo hii kina dada wengi hawaziheshimu ndoa za kaka zao, kisa eti hawamtaki wifi yao, unajua kinachowatokea katika ulimwengu wa roho? Wanapigwa na ukoma! Ndio maana wengi hawasongi mbele, iwe kwenye uchumi nk, wanabeba laana bila wao kujua.

Ukisoma maandiko kwa kutulia utagundua kuwa Mungu anaheshimu ndoa sana, na hapendi kuona matatizo kwenye ndoa yoyote ile. Mungu yupo tayari kumtenga mtu na hata kutoipokea sadaka yake kwa sababu tu, huyo mtu haiheshimu ndoa yake. Sikiliza maneno haya.

"Bwana atamtenga mtu atendaye hayo; yeye aliye macho, na yeye ajibuye, atamtenga na hema za Yakobo, pia atamtenga yeye amtoleaye Bwana wa majeshi dhabihu. Tena mnatenda haya nayo; mnaifunikiza madhabahu ya Bwana kwa machozi, kwa kulia na kuugua, hata asiiangalie tena hiyo dhabihu, wala kuitakabali mikononi mwenu na kuiridhia. Lakini ninyi mwasema, ni kwa sababu gani? Ni kwa sababu Bwana amekuwa shahidi kati ya wewe na mke wa ujana wako, uliyemtenda mambo ya hiana, angawa yeye ni mwenzako, na mke wa agano lako. Hakuna mtu mmoja aliyetenda hivi. Ambaye alikuwa na ufahamu kidogo. Au je! Kuna mtu mmoja atafutaye mzao mwenye kumcha Mungu? Kwa hiyo jihadharini roho zenu; mtu awaye yote asimtende mke wa ujana wake mambo ya hiana. Maana mimi nakuchukia kuachana, asema Bwana, Mungu wa Israeli; naye aifunikizaye nguo yake kwa udhalimu namchukia, asema Bwana wa majeshi; basi jihadharini roho zenu, msije mkatenda kwa hiana." (Malaki 2:12-16)

Umeyasikia maneno hayo? Anasema, Mungu anamtenga na hatapokea sadaka (dhabihu) ya mtu mwenye tabia ya kutoiheshimu ndoa yake. Ona hapo kasema na wanaume waziwazi. Anasema, jihadharini roho zenu, kwa maana nzuri hiyo ni habari ya maonyo kwa kila mwanaume. Anasema, mtu mwenye ufahamu angalau kidogo asingemfanyia mkewe mambo ya hiana au kwa maana nzuri mambo mabaya. Ikiwa wewe mwanaume hauiheshimu ndoa yako Mungu alisha kutenga siku nyingi. Inawezekana kabisa kanisani kwako hawajakutenga, lakini Mungu amekutenga kwa sababu tu, umekuwa jeuri kwenye ndoa yako. Swali langu kwako; wewe ukoje?

Mbona Mungu anaona katika madhabahu yake machozi na kilio cha mkeo au cha mumeo? Unafikiri ikiwa leo hii Mungu amekuchukia siku utakapo kutana naye itakuwaje? Leo hii Machozi ya mkeo au mumeo yanakuzuilia baraka zako. Yaani hata ukitoa sadaka ili akubariki hazipokei sadaka hizo. Je! Akikutemea mate kama alivyomtemea Miriamu unafikiri atakua anakuonea? Sikia, Mungu anasema mtu amfanyiaye mkewe

mambo ya hiana Mungu anamchukia, je! Wewe Mungu anakupenda au anakuchukia? Jijibu mwenyewe. Fikiri jinsi unavyofanya, huiheshimu ndoa yako, unatembea na wanawake wengine nje ya ndoa yako, pia hata wewe mwanamke haujaiheshimu ndoa yako unatembea na wanaume wengine nje ya ndoa yako. Hata wewe dada ona namna ulivyo, haujaiheshimu ndoa ya mtu, unatembea na Mume wake unafikiri sifa, Mungu atakutemea mate kama alivyomtemea Miriamu. Na utabeba laana itakayo kusumbua wewe na uzao wako. Na pia inawezekana umekuwa jeuri na mkatili kwa mkeo na wewe mama ni jeuri sana kwa mumeo fahamu Mungu anakuchukia, tubu, acha tabia hiyo.

Usipoacha hiyo tabia yako mbaya, naamini atakutenga na kukutengenezea jela fulani kama alivyomfunga Miriamu. Siwezi kujua kwako wewe ni jela gani atakayokutupa labda ni ya ukimwi, kansa au mapepo nk. Nakushauri achana na huyo mume wa mtu, kwani kilio cha mke wake kimesikika mbinguni, kama ni mwanaume achana na huyo mwanamke, iheshimu ndoa yako kwani kilio cha mkeo kimesikika mbinguni. Nataka kukuambia bila kukuficha Mungu hakupendi anakuchukia kwa sababu hujaiheshimu ndoa ya mtu. Hata wewe mama na wewe baba na wewe dada na wewe kaka, angalia jinsi mnavyoivuruga ndoa ya huyo ndugu yenu, kwa sababu zenu binafsi, Mungu anaichukia hiyo tabia yenu mbaya, nawashauri tubuni, msiingilie maisha ya ndoa ya huyo ndugu yenu. Sikiliza mwanamke wewe, je! Unaiheshimu ndoa yako? Mbona unasababisha maumivu makali moyoni mwa mumeo? Mungu anaichukia sana hiyo tabia yako mbaya uliyo nayo ya uzinzi kiburi na nk. Fikiri, Mungu kakupa mume na wewe unamvunjia mumeo heshima kwa kulala na mwanaume mwingine, unajua, Mungu anakuchukia sana, badilika, kabla hajakutemea mate usoni, kama alivyomtemea Miriamu. Utapata aibu siku si nyingi, aibu ambayo itapelekea utengwe hata na jamii nakuambia. Jifunze kuiheshimu ndoa yako.

HAKIKISHA HAMUACHANI

Mungu anasema anachukia kuachana, kuna neno kuachana na neno kutengana, watu wengi wameyachanganya hayo maneno mawili. Maneno hayo yana maana mbili tofauti. Kutengana ni pale wanandoa wanapo kuwa mbali kila mtu na mwenzake, na jambo hilo linakuwa wazi, yaani kila mtu anajua kuwa kumetokea nini katika ndoa ya fulani. Kuachana kunaweza kuwa ni siri. hakuna anaye fahamu, hata mumeo au mkeo na jamaa zako wasijue kabisa kuwa umemuacha mumeo au mkeo, ona mfano huu.

"Naye Yusufu, mumewe, kwa vile alivyokuwa mtu wa haki, asitake kumwaibisha, aliazimu kumwacha kwa siri." (Mathayo 1:19)

Yusufu aliamua kumwacha Mariamu kwa siri. Kumbe upo uwezekano kabisa ukaamua kumwacha mkeo au mumeo kwa siri, yaani hata yeye asijue kuwa kaachwa. Mungu anasema anachukia kuachana. Kumbuka kutengana kunatokea baada ya kuachana. Hebu jiangalie ulivyo leo hii, je! Haujamuacha mumeo au mkeo? Ngoja nikupe kipimo

hiki ujipime ndio utagundua umemuacha au la. Mbona unamawazo kuwa ulikosea kuoa au kuolewa? Kama unamawazo kuwa ulikosea, basi tayari umemuacha huyo uliye naye, ni kweli umezaa naye watoto mnalala kitanda kimoja lakini una mawazo na umepokea kuwa ulikosea kuoa au kuolewa na huyo ndugu. Kwa maana nyingine yupo ambaye unafikiri ndiye aliyefaa kukuoa au kuolewa naye. Unajua ukiwa ni mtu mwenye sifa hizo, unakuwa umemwacha huyo mumeo au mkeo. Mungu anachukia kuachana.

Ona zamani ulikuwa na ujasiri wa kuongozana na mkeo au mumeo, mbona sasa hivi hunaujasiri huo tena? Unajua ni kwanini? Umemuacha kwa siri! Zamani mama ulikuwa unapata taabu sana mumeo akisafiri, lakini sasa hivi, akisafiri unapiga magoti na kumshukuru sana Mungu kuwa asante kwa huyo ndugu kupata safari, akikutaarifu kuwa atachelewa kurudi wewe una mwambia Mungu akutie nguvu, kumbe hupendi arudi kabisa! Ukiwa ni mtu wa tabia hiyo fahamu tayari ulishamwacha mwenzi wako. Mbona zamani ulipenda kukaa naye karibu hata kanisani mlikuwa na kawaida ya kwenda wote nk. sasa hivi hutaki kabisa, unajua hizo ni dalili kuwa umemuacha, nakushauri, mrudie mkeo au mumeo. Kwani Mungu anachukia kuachana. Badilika, usikubali shetani akutenganishe na Mungu kwa kukuletea tabia hiyo ya kumuacha mkeo au mumeo.

NDOA NI MPANGO WA MUNGU NA MUNGU NIYE MWANZILISHI WA NDOA

Kwanini leo hii ndoa nyingi zina matatizo kiasi cha kupelekea wanandoa wengi sana kuachana? Sababu kubwa ni hii, shetani ndiye chanzo cha matatizo ya ndoa nyingi sana. Watu wengi kunapotokea matatizo kwenye ndoa zao haraka sana huwaangalia wake zao au waume zao na kuwalaumu kuwa wao ndio chanzo cha matatizo hayo. Kwanini shetani anaziharibu ndoa? Ni kwasababu anafahamu kuwa ndoa ni mpango wa Mungu na Mungu ndiye mwanzilishi wa ndoa.

Mungu ndiye mwanzilishi wa ndoa, na pia anaziheshimu sana ndoa za watu, kwa kuwa Mungu anaheshimu ndoa na ndiye aliyeianzisha ndoa, adui anatafuta kumuudhi kwa kupeleka tabia mbaya kwa baadhi ya wanandoa ili wagombane na kuachana. Mungu ndiye mwanzilishi wa ndoa, na ndoa ya kwanza kabisa ilifungwa mbinguni. Ukisoma maandiko utagundua kuwa, Mungu aliianzisha ndoa huko mbinguni. Tazama maneno haya ya Bwana yasemavyo.

"Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwuumba mwanaume na mwanamke aliwaumba Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia zaeni mkaongezeke, mkaijaze, na kuitiisha; mkatawale samaki wa baharini , na ndege wa wa angani na....."(Mmwanzo 1:27-28)

Ukiyaangalia maneno hayo ya Bwana utagundua kuwa ndoa ilianza kufungwa huko Mbinguni, Kwanini nasema hivyo? Ni kwa sababu, hii; Mungu ni Roho, anaposema na tufanye mtu kwa mfano wetu maana yake aliwaumba kama yeye alivyo yaani ziliumbwa

roho mbili kwa mfano wa Mungu. Na roho hizo ziliumbwa siku moja, yaani mtu mume na mtu mke. Alipowaumba hao wawili siku ile akawaambia wazaane waijaze nchi na watawale vitu vyote.

Ninachotaka uone ni hiki, Mungu yupo mbinguni, na hao waliumbwa kwanza kwenye ulimwengu wa roho yaani huko mbinguni, kumbuka waliumbwa kwanza kwa mfano wa Mungu ambaye ni Roho

"Mungu ni Roho nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli." (Yuhana 4:24)

Mungu na malaika zake waliishangilia siku ile ndoa ya Adamu na mkewe Hawa huko mbinguni kabla hata hajawaleta hapa duniani au katika ulimwengu huu unaoonekana. Hata alipomtanguliza Adamu hapa duniani, alimpatia mke. Nilichotaka ukione ni hiki ndoa ni mpango wa Mungu na Mungu ndiye mwanzilishi wake. Adui analijua hili ndio maana anapigana usiku na mchana ili aziharibu ndoa na anapofanya hivyo na kufanikiwa kuziharibu anajua kuwa anamuudhi sana Mungu na anachotaka ni kuona kila kitu alichokiumba Mungu kinaharibika. Kumbuka shetani ni adui wa Mungu na vitu vya Mungu. Sasa sikia, wewe unapokubali kufanya mambo mabaya katika ndoa yako fahamu unashirikiana na shetani kumuudhi Mungu. Swali langu kwako ni hili, je! Wewe upo upande gani? Tazama Yesu asemavyo.

"Mtu asiye pamoja nami yu kinyume changu; na mtu asiyekusanya pamoja nami hutapanya" (Mathayo12:30).

Wewe ukoje? Ndoa yako umeikusanya yaani mpo pamoja na mkeo au mumeo? Au ndio umeivuruga au kuitawanya vipandevipande?. Jiulize, na kama umekosea nakushauri leo hii utubu, itengeneze njia yako ili uwe pamoja na Mungu usiwe upande wa shetani.

MAMBO MUHIMU UNAYOTAKIWA KUYAFANYA ILI KUILINDA NA KUIPONYA NDOA YAKO

Baada ya kujifunza eneo la Ndoa ni mpango wa Mungu na Mungu ndiye mwanzilishi wa ndoa. Hebu tuanze kuangalia mambo muhimu ambayo unatakiwa uyafanye ili upate kuilinda na kuiponya ndoa yako. Yapo mambo mengi sana, lakini yale ambayo Mungu amenijalia kuyafahamu ndiyo ntakayo yaachilia ili upate kuyafahamu. Na ukiisha kuyafahamu anza kuyafanyia kazi, hapo ndipo utakapoona mabadiliko makubwa katika ndoa yako.

JAMBO LA KWANZA: MRUHUSU MUNGU AITAWALE NDOA YAKO

Siku moja usiku, Mungu aliniwekea neno hili moyoni mwangu, aliniambia Steven, ndoa

nyingi sana zina matatizo. Na akanifundisha kuwa chanzo kikubwa cha hayo matatizo ni kwa sababu wanandoa wengi hawajamruhusu Mungu awatawale, au niseme hivi, ndoa nyingi hazijatawaliwa na Mungu. Kama kuna kitu kikubwa anachotamani Mungu akifanye na ni halali yake akifanye ni hiki cha kutawala kila kitu kilicho duniani, mbinguni na hata chini ya nchi. Siku moja wanafunzi wa Yesu walimuomba Bwana Yesu awafundishe kusali, katika mafundisho yake aliyoyatoa alisema maneno haya.

"Basi salini hivi; Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe leo riziki yetu. Utusamehe makosa yetu kama nasi tuwasamehevyo wadeni wetu. Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu… [kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele] Amina." (Mathayo 6:9-13).

Ukiyasoma maneno hayo utagundua hapo ndani kuna vitu vingi sana ambavyo ndio msingi mkubwa wa maisha ya mwanadamu na mambo yake yote. Bwana Yesu anatufundisha anasema, tumuombe Mungu aulete Ufalme wake hapa duniani. Anaposema salini hivi Ufalme wako uje maana yake haupo! Ili uje inatakiwa wewe umuombe aulete, kama hauta mwambia aulete fahamu hata uleta! Neno ufalme ni tofauti na neno mfalme. Neno ufalme maana yake ni eneo linalotawaliwa na mfalme, neno ufalme maana yake nzuri ni serikali ya mfalme ndiyo inayomiliki na kutawala kwa kuweka utaratibu wake, ambao unapaswa kufuatwa na wale wanaotawaliwa na huyo mfalme katika eneo alitawalalo mfalme. Naamini umenielewa hapo. Sasa kama unataka leo hii ndoa yako iwe salama, lazima uhakikishe unamruhusu Mungu aulete ufalme wake katika hiyo ndoa yako ili ipate kutawaliwa na Mungu Baba wa Mbinguni.

Ukiziangalia ndoa nyingi utagundua kuwa hazitawaliwi na Mungu, yaani ufalme wa Mungu haujaruhusiwa kwenye hizo ndoa, haijalishi wanandoa hao walifunga ndoa kihalali kabisa na kupokea baraka kutoka kanisani, haijalishi hao wana ndoa wameokoka wote au mmoja wao nk. Unaweza kujiuliza swali kwanini unasema hivyo mwalimu? Sikiliza; watu wengi sana wanaomba sana Mungu azilinde ndoa zao lakini kila kukicha utaona jinsi ndoa hizo zinavyobomolewa na adui shetani, wengine ndiyo wanakimbilia kwa waganga wa kienyeji nk. lakini kila siku ni matatizo tu. Unajua ni kwanini ndoa yako haina amani, furaha, nk? Ni kwa sababu haujamruhusu Mungu aitawale ndoa yako! Ninaposema Ufalme wa mbinguni hautawali ndoa yako unaweza ukapata shida sana, ngoja nikuoneshe maana halisi ya neno ufalme wa mbinguni ni nini na hapo ndiyo utaelewa nina maana gani nisemapo Ufalme wa mbinguni hauitawali ndoa yako. Angalia maneno haya ndio utaelewa kuwa ndoa yako inatawaliwa na ufalme upi.

"Maana ufalme wa Mungu si kula wala kunywa, bali ni haki na amani na furaha katika Roho Mtakatifu." (RUM 14:17)

Ukiyaangalia maneno hayo utaona maana halisi ya neno ufalme wa Mungu ni nini. Neno

linasema ufalme wa Mungu ni Haki. Kwenye kitabu cha Isaya, Mungu anatufundisha haki ina kazi gani na ina matunda gani au mazao gani. Ona maneno haya ya Mungu yanavyoizungumzia Haki ilivyo.

"Na kazi ya haki itakuwa amani; na mazao ya haki yatakuwa ni utulivu na matumaini daima." (Isaya 32:17)

Sikiliza, utakapo mruhusu Mungu aitawale ndoa yako lazima ukubaliane na utaratibu wa serikali yake, serikali ya mbinguni yenyewe utaratibu wake wa kwanza ni kuhakikisha Haki ndiyo inayotawala eneo hilo uliporuhusiwa ufalme wa Mungu uje. Ndoa nyingi zimepoteza amani, unajua ni kwanini? Ni kwa sababu Haki haijapewa nafasi ya kutawala hizo ndoa! Sikiliza, ikiwa wewe mwanaume haumtendei mkeo Haki, fahamu amani, furaha, utulivu na matumaini kwenye hiyo ndoa havitakuwepo kabisa. Hata wewe mwanamke ikiwa haumtendei mumeo haki, fahamu amani, furaha, utulivu na matumaini katika ndoa yako havita kuwepo kabisa. Mtajikuta mkigombana na kupoteza matumaini na utulivu na furaha itatoweka tu. Kama mtakimbilia kumuomba Mungu awaletee amani, atakacho wafundisha ni hiki cha kila mmoja wenu ahakikishe anakubali haki itawale katika hiyo ndoa. Yaani uhakikishe unatenda matendo ya haki kwa mwana ndoa mwezio. Kinyume cha hapo msitarajie amani, furaha na matumaini kwenye hiyo ndoa yenu, haijalishi mmeokoka au ni watumishi wa Mungu nk. Watu wengi hawajui Ufalme wa mbinguni ni nini, wengi wanaomba ufalme wa mbinguni uje kwenye ndoa yao, nchi yao, ofisini kwao nk, hawajui kuwa ukija huo ufalme utakacholeta ni Haki. Yaani kila mmoja ahakikishe anamtendea kila mtu matendo ya haki, yaani kama ni ofisini wewe bosi lazima uwape hao watumishi wako haki zao, ukiwanyima tu, unakuwa unashindana na haki, hapo haki itakachofanya ni kuondoa amani na utulivu, ndipo unaposikia wamegoma, wameiba nk. Hata kwenye ndoa ni hivyo hivyo.

Haki ina matendo yake, yanaitwa matendo ya haki ona maneno haya ya Bwana yasemavyo.

"Na tufurahi, tukashangilie, tukampe utukufu wake; kwa kuwa arusi ya mwana-kondoo imekuja, na mkewe amejiweka tayari. Naye amepewa kuvikwa kitani nzuri, ing'arayo, safi; kwa maana kitani nzuri hiyo ni MATENDO YA HAKI ya watakatifu". (UFU19:7-8)

Haki inamatendo si maneno na kuamini tu, sikiliza, leo hii utamuomba Mungu aulete Ufalme wake katika ndoa yako hiyo, yaani unakubali akutawale, jambo la kwanza lazima ukubali kuanza kuyatenda matendo ya HAKI. Ngoja nikupe mifano hii ndiyo utaelewa ni nini ninacho kizungumzia. Wewe mwanamke umepewa mume huyo, huyo anazo haki zake kama mume ambazo wewe mwanamke unatakiwa uhakikishe unamtedea, mume ni kichwa, kama ni kichwa neno la Mungu linasema ni mtawala, mpe haki yake ya kukutawala! Usipokubali tu, fahamu amani utulivu na furaha vitatoweka tu, hata ufunge na kuomba sana, nina maana hii, ondoa kiburi ulicho nacho kwa mumeo, mtii na hiyo

ndiyo haki yake. Nini iliyo haki ya mumeo? Iruhusu kwa kuitenda si kwa maneno ndipo utakapoona ulinzi kutoka kwa Mungu ukikulindia ndoa yako.

Hata wewe mwanaume, umepewa huyo mwanamke, ana haki zake kama mkeo, haki ya mwanamke ni msaidizi wako, neno msaidizi Kibiblia ni pana sana. Si kukufulia nguo na kukupikia tu, ni zaidi ya hapo. Ni haki ya mkeo ajue na afahamu wewe unafanya kazi gani, unakipato cha kiasi gani, anatunzwa na wewe, nk. Wanaume wengi hawaoni kuwa kwa kutowashirikisha wake zao kwenye eneo la kipato chao hawawatendei haki kabisaa. Kutokana na tabia hiyo, hapo ndipo ugomvi unapotokea na furaha kuondoka kwa mkeo nk. Sikiliza mpendwa kama unataka Mungu akutawale ruhusu haki itawale katika ndoa yako! Mpe heshima mkeo hiyo ndiyo haki yake, mtunze hiyo ndiyo haki yake, watu wengi hawajui kuwa ni haki mke kuheshimiwa na mumewe ona maneno haya ya Mungu yasemavyo. “kadhalika ninyi waume, kaeni na wake zenu kwa akili; na kumpa mke heshima, kama chombo kisicho na nguvu; kama warithi pamoja wa neema ya uzima, kusudi kuomba kwenu kusizuiliwe.” (1Petro 3:7).

Haki inataka kukuona wewe mwanaume unamheshimu mke, unaweza kuniambia kuwa kwa kitendo chako cha kutokumpa mkeo habari za kipato chako, unamficha kitabu chako cha benki, je unatenda haki? Wewe angalia unapopata mshahara je! Unamuonyesha mkeo na mnakaa na kupanga mfanye nini? Kama haufanyi hivyo nakuambia ukweli hautendi matendo ya haki, kumbuka haki ikiondoka amani inaondoka na furaha inaondoka kuna baki magomvi na machungu. Sikia wewe mwanamke, ikiwa leo mumeo amekuletea fedha na akakupa fedha hizo kwa ajiri ya matumizi fulani, harafu wewe bila kutaka ridhaa ya mumeo unakwenda sokoni kununua nguo zako, sahani, heleni, mafuta uzuri, nk, wakati alikupa fedha hizo kwa ajiri ya matumizi ya mboga, mahindi, au kulipa deni la maji umeme nk, kwa kufanya hivyo unakuwa unamtendea mumeo haki? Sikia kwa kufanya hivyo utakuwa hautendi haki.

Kwa kuwa hujaitenda haki, fahamu kitakacho tokea ni ufalme wa giza kuitawala ndoa yako, yaani ugomvi na huzuni itawatawala tu. Kwa mifano hiyo michache umeelewa nina maana gani ninapozungumzia habari za Ufalme wa Mungu kuitawala ndoa yako. Ukiziangalia ndoa nyingi utagundua hazitawaliwi na Mungu, kwa sababu haki haijapewa nafasi katika hizo ndoa.

Wanaume wengi leo hii, wanazini, kwa kufanya tendo hilo wanakuwa hawawatendei haki wake zao, na Mungu pia, kwa kufanya hivyo tu tayari ufalme wa giza unaanza kuitawala ndoa hiyo, hapo ndipo shetani anapoachilia magomvi, anaondoa furaha, na utulivu uliokuwepo kwenye ndoa unaondoka. Furaha iliyokuwa kwa mkeo inapotea kabisaa. Na kuirudisha ni gharama kweli na kuambia. Hata baadhi ya wanawake wanazini nje ya ndoa, kwa kufanya hivyo, hawawatendei waume zao haki na Mungu pia. Kwa kutomtendea mumeo haki yake kwa kugawa penzi ambalo ni haki ya mumeo na kumpa mwanaume mwingine nakuambia ukweli amani itatoweka tu kwenye hiyo ndoa

yako mama, na kuirudisha unahitaji kugharamia sana.

Haki ina taka hivi “Ndoa na iheshimiwe na watu wote, na malazi yawe safi; kwa maana waasherati na wazinzi Mungu atawahukumia adhabu.” (EBR 13:4). Haki imeagiza ndoa na iheshimiwe na watu wote, wewe mwanaume ni mtu, na wewe mwanamke ni mtu, mumeagizwa kila mmoja ahakikishe hafanyi uzinzi. Ona jinsi wewe ndugu yangu leo hii ulipoangukia, umesukumia haki mbali, kwa kutoiheshimu ndoa yako kwa kuzini na mwanamke mwingine na hata wewe mwanamke umefanya hivyohivyo, sikiliza Mungu atakuadhibu, kwanini atakuadhibu? Kwa sababu umeikataa haki, haki ndio utaratibu wa serikali yake, wewe umeikataa isikutawale, umekubali kutawaliwa na ufalme wa giza, ndio maana wewe mwenyewe umepoteza furaha, amani, hata matumaini ndani ya moyo wako.
Sikiliza mpendwa leo unao uwezo wa kuanza maisha mapya yaliyojaa matumaini au mwangaza wa nuru mpya kutoka mbinguni katika ndoa yako hiyo kwa kufanya jambo moja tu. Nalo ni hili, omba ufalme wa mbinguni uje kwenye ndoa yako! Mwambie Mungu aje aitawale ndoa yako, usiogope Tubia makosa yako, geuka yaache yale ya zamani, ndoa yako itaponywa na kulindwa kabisaa.

Mruhusu aje sasa hivi, atakusamehe, na ataanza kuitawala hiyo ndoa yako, acha mambo yote uliyokuwa unayafanya ambayo haya kuwa ya haki. Anza kumtedea mkeo au mumeo matendo ya haki, Mwamini Yesu kama Bwana na mwokozi wako, mpokeeni Yesu katika mioyo yenu kwa imani, nawaambia ukweli ndoa yenu ndipo itakapo pata amani na usalama mkubwa sana, fanyeni maombi, samehaneni, sikiliza haki ikitawala, itataka kuona kila mmoja wenu akimsamehe mwezie pale alipomkosea na hata atakapokosea baadaye. Haki ikiwatawala itawatengenezea ndani ya mioyo yenu moyo wa toba. Kila mmoja wenu atakuwa tayari kumwambia mwenzie nimekosa, mwanaume utakuwa tayari kumwambia mkeo nisamehe, nimekukosea, na mwanamke pia utakuwa tayari kumwomba mumeo msamaha mahali pale ulipomkosea. Na muwe tayari kusamehana.

Sikiliza Haki inavyotaka nyinyi wanandoa mfanye kila siku kama mnataka Mungu awatawale ni haya yafuatayo. “Kadhalika ninyi waume, kaeni na wake zenu kwa akili; na kumpa mke heshima, kama chombo kisicho na nguvu; kama warithi pamoja wa neema ya uzima, kusudi kuomba kwenu kusizuiliwe. Neno la mwisho ni hili;mwe na nia moja, wenye kuhurumiana, wenye kupendana kama ndugu, wasikitivu, wanyenyekevu; watu wasiolipa baya kwa baya, au laumu kwa laumu; bali barikini; kwa sababu hayo ndiyo mliyoitiwa ili mrithi baraka.” (1PETRO 3:7-9).

Ndugu yangu nakusihi sana usikiapo maneno hayo, yaweke kwenye matendo. Mruhusu Mungu awatawale kwa kuuleta Ufalme wake katika hiyo ndoa yenu. Pia kubalini kuishi sawasawa na utaratibu uliomo ndani ya ufalme wa Mungu ambao ni HAKI. Tendeaneni matendo ya haki, hapo haki itatenda kazi ya kuleta amani, na itazaa furaha, matumaini mapya na utulivu katika ndoa yenu.

JAMBO LA PILI: MUWE WABUNIFU KATIKA SUALA LA MAPENZI (MSIONEANE HAYA)

Moja ya jambo ambalo ndiyo kiini cha matatizo kwenye ndoa nyingi ni hiki cha wanandoa wengi kutokuwa na ufahamu mkubwa wa suala zima la mapenzi au niseme mahaba. Watoto wa Mungu wengi sana hawana elimu toshelevu katika eneo hili. Neno la Mungu linasema wazi kuwa kila mwanandoa lazima ahakikishe anampatia mwenzie haki yake. Ona, "Lakini kwa sababu ya zinaa kila mwanamume na awe na mke wake mwenyewe, na kila mwanamke na awe na mume wake mwenyewe. Mume na ampe mkewe haki yake, vivyo hivyo mke na ampe mumewe haki yake. Mke hana amri juu ya mwili wake, bali mumewe; vivyo hivyo mume hana amri juu ya mwili wake, bali mkewe .msinyimane isipokuwa mmepatana kwa muda, ili mpate faragha kwa kusali; mkajiane tena, shetani asije akawajaribu kwa kutokuwa na kiasi kwenu." (1KOR 7:7-5)

Ukiyaangalia maneno hayo utagundua kuwa wanandoa wamepewa amri ya kuhakikisha kila mmoja anahakikisha anampa mwenzie haki yake ya kimapenzi au mahaba. Neno linasema wazi kuwa mwenye amri juu ya mwili wa mwanaume ni mke wake, na mwenye amri juu ya mwili wa mke ni mumewake. Siku Mungu ananifundisha somo hili. ALISEMA NAMI WAZIWAZI NA KUNIONYESHA JAMBO HILI JINSI LILIVYO NA AKANIAMBIA WAZI KUWA TATIZO KUBWA LINALOPELEKEA NDOA KUWA NA SHIDA LIPO HAPO. Wanandoa wengi, hawako huru katika suala hili la mapenzi, wengi ni waoga, na wenye aibu sana kwa wake zao au kwa waume zao. Nilikuwa na maswali mengi sana mojawapo ni hili, kwanini wanandoa wengi wanatoka nje ya ndoa? Kwa nini wakitoka hawaludi kwa wake zao? Au kwa waume zao? Kwanini wanawake walioolewa wanapata taabu sana kwa sababu waume zao hawawajali na hawataki kuwatunza tena?

Mungu alinijibu maswali yangu hayo yote, kwa kunifundisha kuwa, tatizo lipo kwa wanawake walio ndani ya ndoa,. Hasa Wakristo, hawana elimu ya suala hili la mapenzi, ngoja nikupe mifano hii labda ndiyo utaelewa. Neno la Mungu linasema, malaya hawawaonei haya au aibu waume za watu, na hiyo ndiyo silaha yao kubwa sana wanayoitumia. Ona maneno haya.

"....Nikaona katikati ya wajinga, nikamtambua miongoni mwa vijana, kijana mmoja asiyekuwa na akili, akipita njiani karibu na pembe yake, akiishika njia iendayo nyumbani kwake. Wakati wa magharibi, wakati wa jioni, usiku wa manane, gizani. Natazama, mwanamke akamkuta, anamavazi ya kikahaba, mwerevu wa moyo; anakelele, na ukaidi; miguu yake haikai nyumbani mwake. Mara yu katika njia kuu, mara viwanjani, naye huotea kwenye pembe za kila njia. Basi akamshika, akambusu, akamwambia kwa uso usio na HAYA. Kwangu ziko sadaka za amani; leo hivi nimeziondoa nadhiri zangu; ndiyo maana nikatoka nikulaki, nikutafute uso wako kwa bidii, nami nimekuona. Nimetandika kitanda changu, magodoro mazuri, kwa matandiko ya Kimisri yenye misitari. Nimetia kitanda changu manukato, manemane na uudi na mdalasini. Haya tushibe upendo hata

asubuhi, tujifurahishe nafsi zetu kwa mahaba. Maana mume wangu hayumo nyumbani, amekwenda safari ya mbali; amechukua mfuko wa fedha mkononi; atarudi wakati wa mwezi mpevu. Kwa maneno yake mengi na ulaini akamshawishi kwa ubembelezi wa midomo yake akamshinda." (MITHALI 7:6-21)

Ukiyasoma maneno hayo utaona ni kwanini wanawake wengi leo hii ndoa zao zimewashinda. Ona mwanamke huyo alimpata huyo kijana kwa sababu alikuwa mjanja sana kwenye masuala ya mapenzi, kuanzi kuvaa kwake, kusema kwake, na neno linasema mwanamke huyo hakuwa na haya au aibu kabisa. Alimfuata huyo mwanaume akambusu, akaanza kumweleza huyo mwanaume maneno yaliyojaa mahaba kweli, ona huyo kijana, neno linasema kwa maneno mengi ya kimapenzi yaliyo laini yakamshawishi huyo kijana akaenda na huyo mwanamke, ona mwenyewe neno linasema "Kwa maneno yake mengi na ulaini akamshawishi kwa ubembelezi wa midomo yake akamshinda". Nataka nikuulize swali hili wewe mwanamke, je! Wewe ukoje kwa mumeo? Mbona huna muda wa kumbembeleza mumeo kwa maneno laini, ya kimapenzi? Wewe unajua kumdai fedha ya kula na kukununulia nguo tu, nk. Lakini haumpi mumeo haki yake ya kimapenzi kisasawa. Unajua siku akikutana na mwanamke mjuzi na mbunifu wa mapenzi nakuambia ukweli, mumeo hawezi kukurudia. Sikia akikutana na mwanamke wa namna hiyo hata akiwa na wewe hatakutunza, yaani hata kupa mahitaji yako kama mwanzo, Kwanini? Ni kwasababu akili zake zote zina hamia huko kwa mwanamke huyo mtundu wa masuala ya mapenzi.

Mungu analijua hilo ndio maana anatufundisha hivi.

"Usiutamani uzuri wake moyoni mwako; wala usikubali akunase kwa kope za macho yake. Maana kwa malaya mtu hutiwa katika hali ya kuhitaji kipande cha mkate; kahaba humwinda mtu anase nafsi yake iliyo ya thamani."(MITHALI 6:25-26)

Neno la Mungu linasema mtu yoyote yule ambaye amekutana na mwanamke mjunzi wa mapenzi ambao wengi wao ni malaya kwa sababu wao hutafuta sana wanaume za watu, hapo ndipo wanakuwa wabunifu kila siku wa masuala ya kuwafanyia hao waume za watu kuliko hao wake za watu ambao kwa ujinga wao wamejisahau kwa kujiamini kuwa wameolewa na hawaoni umuhimu wowote wa kubuni, kujituma na hata kutafuta mbinu za kunogesha mapenzi katika ndoa zao.

Neno linasema mwanaume yeyote anayekutana na mwanamke malaya yaani mtundu, uhitaji wake kwa huyo mwanamke unakuwa mkubwa sana. Mungu amemfananisha na mtu aliye na njaa kali ambaye anahitaji angalau kipande kidogo cha mkate ili ale na ashibe. Sikiliza mwanamke wewe Mungu ameyaachilia maneno hayo makusudi ili akufundishe wewe ujue mbinu ya adui yako akuchukuliaye mumeo anavyofanya. Ili na wewe ufanye mara mbili ya adui yako, kama unataka kumlinda mumeo lazima ujue ni silaha gani aitumiayo mwanamke huyo akuiibiaye mumeo. Sikia, moja ya silaha

alizo nazo ni hii, amuonei haya mumeo, na ni mbunifu wa mapenzi kwekweli. Ndio maana mumeo kila wakati anamuwaza huyo mwanamke, kila wakati anamuhitaji huyo mwanamke, wewe hakuitaji tena kisa ni hicho hakuna uchawi mwingine nakuambia. Jitahidini kuwa wabunifu wa masuala ya mapenzi na kutooneana aibu, hakikisheni mnakua huru kwenye suala zima la mahaba. Ninataka nikutie moyo wewe mwanamke haujachelewa, anza kumuomba Mungu akupe akili ya kuyafahamu yale unayotakiwa uyafanye katika jambo hili la mapenzi kwa Mumeo. La muhimu usimuonee haya mume. Hata wewe mwanaume pia hivyohivyo hakikisha unakua mbunifu kwenye suala hili la mapenzi usimuonee haya mkeo. Umenielewaaa? Ni aibu mkeo aseme awaze wanaume wengine wakati wewe upo!

Ebu tusogee mbele kidogo kwenye kona hii ambayo ni muhimu sana kwa kila mwanandoa. Ili leo hii ndoa yako iwe salama uhakikishe unalitazama jambo la mahaba kwa mtazamo tofauti kabisa. Wanandoa wengi sana, wanafikiri jambo hilo ni dhambi, ndio maana hawatafuti maarifa ya namna ya kulifanya liwe bora sana katika ndoa yao. Wengi wanapo kuwa na wake zao au waume zao hawawezi kuwa huru kwa sababu fikra zao zinakimbilia kufikiria kuwa wanakosea, ndio maana wengi wanapofanya tendo la ndoa wanafanya pasipo kutulia akili zao, hata kuwa busu wake zao au waume zao wanaogopa , wengi wakifanya wanakimbilia kutubu, wanaomba msamaha Mungu awasamehe, Siliza ndugu, suala la mapenzi kwa mkeo au mumeo ni takatifu kwa Bwana. Fanya bila hofu wala haya, tena Jifunzeni hata kumkaribisha Roho Mtakatifu awe na nyinyi katika muda huo mnapokuwa katika hali ya mapenzi.

Sikiliza neno la Mungu lina sema hivi. “Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi; akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hawezi kufanya neno lolote.” (YOHANA 15:5). Ukiyasoma maneno hayo kwa kutulia utagundua wazi kuwa, wewe na mimi hatuwezi kufanya jambo lolote lile. Mpaka tumewezeshwa kulifanya na Yesu Kristo aliye mwanzilishi wa mambo yote, na mojawapo ni hili la mapenzi katika ndoa. Yeye ndiye analijua na kulifahamu, yeye ndiye anajua nini kinatakiwa kifanyike kwa wakati gani, katia suala zima la mapenzi kwa wana ndoa. sasa unapo jifunza kutafuta msaada kutoka kwake katika jambo la mapenzi nakuhakikishia atakufundisha mambo mengi sana ambayo huyajui na wala huwezi kuyafanya mpaka akuwezeshe yeye uyajua na uwezeshwe kuyafanya,. Sikiliza yeye atakuletea neno, au mafundisho, iwe kwenye akili zako au kwa kutumia Biblia ama kwa mwalimu wa neno la Mungu. Wanandoa wengi wanafikiria kuwa shetani ndiye mwanzilishi wa jambo hili. Sikiliza mpendwa Mungu ndiye mwanzilishi, alilianzisha na kuliweka kwenye ndoa, amelikataza kwa watu wasio na ndoa wasilifanye, ila wakiwa ndani ya ndoa ni ruksa kulifanya tena kwa ubora sanaaa. Wakristo wengi wanafikiria aliliweka ili kuzaana tu. Sikiliza tendo la mapenzi au tendo la ndoa na mahaba ndani yake Mungu ameliweka akiwa na makusudio mengi sana. Ngoja nikupe haya machache uone.

KUMLINDA MWENZIO NA DHAMBI YA UZINZI

Neno la Mungu linasema wazi kuwa, baada ya shetani kuliharibu tendo hili kwa kuwashawishi watu kulifanya bila kufuata utaratibu kwa kulianzisha mapema kwa watu wajinsia mbili tofauti kujamiana kabla ya kuoana, na hata wakioana wakalifanya nje ya ndoa yao. Mungu aliamua kulifanya jambo la mapenzi au tendo landoa kwa wanandoa liwe ni sehemu ya ulinzi kwa kila mwanandoa.

"Lakini kwa sababu ya zinaa kila mwanamume na awe na mke wake mwenyewe, na kila mwanamke na awe na mume wake mwenyewe. Mume na ampe mkewe haki yake, vivyo hivyo mke na ampe mumewe haki yake. Mke hana amri juu ya mwili wake, bali mumewe; vivyo hivyo mume hana amri juu ya mwili wake, bali mkewe msinyimane isipokuwa mmepatana kwa muda, ili mpate faragha kwa kusali; mkajiane tena, shetani asije akawajaribu kwa kutokuwa na kiasi kwenu." (1KOR 7:7-5).

Ukiyasoma maneno hayo utagundua kuwa tendo la ndoa limewekwa kwa makusudi ya kila mwanandoa alindwe na dhambi ya uzinzi, Sikiliza Mungu alipokupa mke nia yake huyo mkeo akae kama mlizi wako wewe ili usiingie kwenye dhambi ya uzinzi, hata kwako wewe mwanaume ni hivyo hivyo. Sasa ikiwa leo hii wewe mwanamke au wewe mwanaume, Unamuonea aibu mkeo au mumeo na wala haumtoshelezi katika suala la mapenzi(ngono) unafikiri nini kitatokea? Unakuwa unamsababishia mwenzio ajikute anashambuliwa na dhambi ya uzinzi, nina kumbia ukweli kama mmoja wa wana ndoa hatosheki na katika suala zima la mapenzi ndani ya ndoa yake ni rahisi kupatwa na dhambi ya uzinzi. Kwa hiyo ni Lazima hapo uhakikishe mpendwa unakuwa makini kweli kwenye eneo la ubunifu na uchochezi wa mahaba kwa mkeo au mumeo bila kumuonea haya, kwani akiangukia kwenye dhambi hiyo fahamu haujamlinda vema, yaani kuna sehemu umezembea.

Ngoja nizungumze kidogo na wanaume wenzangu, Wanaume wengi leo hii hawataki kujifunza mbinu mbalimbali ili wake zao wawe salama katika eneo hili la uzinzi nk. Sikiliza mara nyingi sana, kinamama ndio wanaoitikia sana wanapotangaziwa kuwa kutakuwa na semina za mafundisho ya somo la ndoa. Kina baba wengi hawaendi kabisaa kwenye semina hizo, hata wakiludi hao wake zao hawawaulizi kuwa mmejifunza nini, ili hata wao wapokee maarifa mapya au wakumbushwe yawapasayo kuyafanya. Kina baba wengi wao wanafikiri wanajua sana suala mapenzi wakati wengi hawajui kitu chochote kile. Wanaume wengi sana kwa sababu ya maumbile ambayo Mungu ametuumbia, ya kuwahi kupata msisimko wa mapenzi kuliko wanawake utaona wengi hawana maarifa ya kutuliza akili zao wanapokuwa katika hali hiyo, wengi wanajikuta wamekabiliwa na muhemko wakiwaona tu wanawake, iwe wanawake waliowaoa, au hao wanaokutana nao barabarani, au kwenye picha nk. Sasa kutokana na tatizo hilo wanaume wengi wanajikuta hawawapi wake zao raha ya mahaba mpaka wakaliona tendo la ndoa kuwa ni takatifu. Wanaume wengi wanawaingilia wake zao bila maandalizi ya kutosha,

wakitumia nguvu kubwa sana, kumbe kwa kufanya hivyo wanakuwa wanawafanya hao wake zao walichukie tendo la ndoa kwa kuwa wao walivyoumbwa na Mungu wameumbwa tofauti na wanaume, wenyewe wanahitaji maandalizi kwa muda mrefu, ndio maana nakuambia wewe mwanaume unatakiwa hapo sasa uwe mbunifu kweli. Katika wanawake mia utakao kutana nao wanawake sabini na tano, hawalitaki tendo la ndoa. Kisa ? wanaumia, sikiliza ndugu jifunze kumundaaa mkeo kwa muda mrefu sana kabla haujamuingilia kimwili. Wana sayansi wanasema mwanamke ili alifaidi tendo la ndoa inatakiwa aandaliwe kwa masaa sita. Unaweza kusema ntafanyaje? Sikiliza, Tafuta michezo ya kucheza naye kimahaba, ongeanaye maneno ya mahaba, usimuonee aibu, ona. Tokea asubuhi mpe taarifa kijanja kuwa leo baadaye unamuhitaji, jifanye hutaki kwenda kazini, akikwambia muda unaenda nenda kazini!, mwambie nataka nikae nawewe, hayo ni maandalizi, ukifika ofisini mtumie ujumbe wa mapenzi kwa njia ya simu. Ebu mwambie kuwa leo uwahi kumaliza kazi zako mapema ili tulale mapema, au mwambie leo sitaki ujichoshe nk. Ukifanya hivyo utakua unamuandaa kiakili mkeo umenielewa sasa?.

Wanaume wengi hawaijui miili ya wake zao kwa sababu wanawaonea aibu, wamewaachia madaktari ndio wanaoijua miili ya wake zao, si wanaenda huko na wanapata tiba huko hospitali, wanavua nguo nuruni ili wachomwe sindano nk. Wenye wake wenyewe hawaijui miili ya wake zao vizuri. Unaweza kusema kivipi mwalimu? Ona kwanza unaharaka kama risasi itokayo kwenye bunduki ya AK47 unapomuingia mkeo. Pili unamuonea aibu, kila unapomtaka unafanyanaye gizani, unazima taa, unafikiri utaujua mwili wa mkeo ulivyo kweli? Hata kuoga unaoga peke yako, sikiliza usimuonee aibu mkeo, mkague kona zote uone ameumbwaje. Ngoja nikupe mfano huu ambao neno la Mungu linatufundisha.

“Nao walikuwa uchi wote wawili Adamu na mkewe, wala hawakuona haya.”
(MWANZO 2:25)

Walikuwa uchi wote wawili bila aibu au haya, wewe ukoje? Njoja nikuulize wewe mama je! unaujasiri wa kukaa uchi mbele ya mumeo na ukajionyesha mwili wako wote jinsi ulivyo? Fikiri malaya wao wanawakaria uchi waume zenu tokea wakiwa barabarani bila haya, wewe waone wanavyo vaa vinguo vya uchi uchi barabarani mchana kweupe, sasa wakiwa chumbani inakuaje? sasa wakikutana nao huko chumbani inakuwaje? Ndio maana Mungu anataka mama uwe mbunifu wa mapenzi nawewe baba pia, muwe huru zungumzeni, fundishaneni, muelekeze mwezio akushike wapi, akukune wapi, mkiwa huru kabisaa, fikiria mkeo bahati mbaya sana kabla wewe haujamuoa alianza kulijua jambo hili mapema sana. Sawa sasa hivi kaokoka na ni mtumishi wa Mungu nk, harafu anakutana na wewe ndugu yangu ndio huna maarifa kabisaa, wewe unajua kuweka tu halafu unamaliza dakika tano, unavaa unaenda bafuni unamuacha hapo ndio kwanza alianza kupata msisimko kama mwanamke, unafikiri akikutana hao wapenzi wake wa zamani ambao ni mafundi kweli kwenye kona hii ya mapenzi atafanya nini?

Nakuakikishia kama hana upako mkubwa ni rahisi sana kuangukia kwenye uzinzi. Hata wewe mwanamke, fikilia huna muda wa kukaa na mumeo na ukamuuliza, na ukajadiliana naye kuhusu suala la mapenzi akuelekeze anataka nini, ukaeje, ufanyeje, umshike wapi, useme nini, nk, fikiri kabla hajakuoa wewe alisha kutana na wanawake kama wewe, lakini mnatofautiana ujuzi wa mapenzi na mahaba, unafikiri anapokuwa na wewe anakumbuka nini? Ikiwa haumshibishi na akashiba vizuri kwako, atakikumbuka sana chakula kile alichokula huko nyuma kabla hajakuoa wewe ni chakula cha ndizi au wali, nazungumza kiutu uzima. Sizungumziii kupika umenielewa mwanamke wewe? wanaume hawaangalii sana mapishi yako ya jikoni wanaangalia mapishi ya kitandani unanielewa dada yangu? Leo wanawake wengi wanalia ndoa zao zinashida kisa ni hiki, si wabunifu katika suala la mapenzi, ni wavivu wa kufikili hata kulifanya kwa ubora. Hawana muda wa kujifunza habari za mapenzi, sikiliza mumeo anataka aone kitu kipya, maneno mapya ya mapenzi, jifunze hata kusema mkiwa wawili kamapenzi siyo dhambi! Cheza naye, bila kumuonea haya. Unaweza kusema ntajulia wapi? Sikiliza baba na wewe mama. Ndani ya neno la Mungu huko utakuta maarifa mengi sana ya namna ya kufanya katika kona hii ya mahaba. Ona mifano hii.

"Ikawa alipokuwa amekaa huko siku nyingi, Abimeleki, mfalme wa Wafilisti, akachungulia dirishani, akamwona Isaka anacheza-cheza na Rebeka mkewe. Abimeleki akamwita Isaka akasema, yakini huyu ni mkeo, mbona ulisema, ni ndugu yangu huyu?" (MWANZO 26:8-9).

Hebu jiulize swali hao mtu na mkewe walichezacheza kamchezo gani ambako, Mfalme huyo aligundua ni mtu mke na mume walicheza mchezo gani? Sikiliza jifunzeni kucheza mtekenye,tekenye! mguse maeneo ya kumsisimua mumeo au mkeo, Tafuteni mitindo ya kulala mfanyapo tendo la ndoa. Sikia ni nyinyi wenyewe mnatakiwa kubuni hiyo mitindo, mwambie ebu lala hivi, ebu fanya hivi! watu wengi wanamtindo wa kifo cha mende tu!

Sikia mama hata huo mtindo hauko ndani ya Biblia, ni ubunifu aliobuni mwanadamu, basi buni na mitindo mingine ili unogeshe mapenzi hasa mfanyapo tendo la ndoa. Huko mbele nimekuwekea baadhi ya mitindo kama ishilini na nane hivi utaiona huko mbele. Ndani ya neno la Mungu kuna mambo mazuri sana ya kila aina, inategemea unataka kujifunza nini, Ona mfano huu, neno la Mungu linatufundisha kuhusu habari za maziwa ya mwanamke, linasema maziwa ya mwanamke ni ya mtoto na baba pia! Si ya mtoto tu. Pia ni kwa ajiri ya mume. Sikiliza haya maneno

"Chemchemi yako ibarikiwe; nawe umfurahie mke wa ujana wako. Ni ayala apendaye na paa apendezaye; MAZIWA YAKE YAKUTOSHE SIKUZOTE na kwa upendo wake ushangilie daima. Mwanangu mbona unashangilia kifua cha malaya na kukikumbatia kifua cha mgeni. (MITHALI 5:18-20).

Ukisoma maneno hayo utagundua kuwa mwanaume anavutiwa na maziwa ya

mwanamke, kwa hiyo wewe mama lazima ujue hilo. Pia mwanaume wewe lazima ujue kuwa maziwa ya mkeo yana sehemu katika eneo la mapenzi. Jifunze kuyashika, kuyatomasa, ili mkeo afurahie mahaba, mama mtunzie mumeo hayo maziwa vizuri, kwani ikibidi atayanyonya ili wewe usisimke vema. Kumbuka maziwa ni mali ya mumeo ili ayachezee! Sikia tena maneno haya ya Bwana yasemavyo .

"Yakulinde na mwanamke mwovu, asikupate.....Usiutazame uzuri wake moyoni mwako; wala usikubali akunase kwa kope za macho yake."(MITHALI 6:24-25).

Umeyasikia maneno hayo wewe mwanamke? Macho yako unaweza kuyatumia kama sehemu ya kuchochea mapenzi kwa mumeo, Mungu anajua kuwa mwanamume anaweza kunaswa katika mapenzi kwa kuyaangalia macho ya mwanamke, sasa unapokuwa na mumeo jifunze kuyafanya macho yako yawe sehemu ya kuimalisha lindo lako ili asiende kuzini nje ya ndoa yako.

Ngoja nikupe mfano huu. Sikia mwanamke wewe, hakikisha unachomoa risasi zote kwenye bunduki ya mumeo. Sikiliza mwanamke aliyeolewa na muwindaji anakili sana ya kujilinda, anahakikisha mume wake aludipo kutoka mawindoni anazichomoa risasi zote ndani ya bunduki, anaye zichomoa ni mwanamke wala si mwanaume. Kwanini anazichomoa? Ni kwa sababu siku mume wake akikasirika anaweza kuitumia hiyo bunduki kumuua. Sasa hata wewe mwanamke, ondoa kila risasi kwa mumeo, hakikisha akiondoka bunduki yake haina risasi kabisaaa. Kwani baba muwindaji akiondoka na risasi na akakosa windo anaweza kujifunza kulengea shabaha kwenye miti, na kupoteza risasi bure, Sikia mumeo atokapo hakikisha hana risasi za kuwapigia machangudoa nk.

Jifunze kusoma maandiko matakatifu, mfano kitabu cha Wimbo ulio bora. huko ndani utaona jinsi Mungu alivyoliachilia neno lake linalohusu mapenzi kati ya wanandoa. Huko utapata mambo mengi, namna ya kumshika mpenzi wako, namna ya kusema maneno ya mahaba nk. Mfano angalia maneno haya

"Siti msharifu, jinsi zilivyo nzuri hatua zako katika mitawalanda. Mapaja yako ya mviringo ni kama johari, kazi ya fundi mstadi; kitovu chako ni kama birauri iliyoviringana, na isikose divai iliyochanganyika;Tumbo lako ni mfano wa chungu ya ngano, iliyozungukwa na ugo wa nyinyoro, maziwa yako mawili ni kama wana-paa wawili ambao ni mapacha ya paa....."(WIM 7:1-3).

Sikiliza neno lingine katika kitabu cha Wimbo Uliobora

"Mkono wake wa kushoto ungekuwa chini ya kichwa changu, nao wakuume ungenikumbatia. "...Nalikuamsha chini ya huo mpera; huko mama yako alikuonea utungu aliona utungu aliyekuzaa"(Wimbo 8:3-4).

Yaangalie kwa makini maneno hayo utaona wazi kuwa kuna maeneo unatakiwa uyashike kwa makini pia ujifunze kumsifia mkeo au mumeo jinsi alivyoumbwa. Ebu jifunze hata kwa bata, sikia, bata hamfuatii kwa haraka bata jike, mpaka amgongegonge kwanza kwa mabawa yake kwa mahaba ndipo anampanda bata jike. Umeelewa mpendwa?

PICHA ZA MITINDO (STYLE) WAKATI WANA NDOA MPO KWENYE TENDO LANDOA

Ngoja nikupe angalau kwa kiasi michoro hii uone namna ambavyo mnaweza kulifanya tendo la ndoa kuwa zuri kwa nyinyi wanandoa, mnaweza kuwa wabunifu zaidi ya hapa.

Hata na nyinyi mnaweza kujiongezeeni michoro yenu zaidi ya hii michache niliyokuwekea hapa. Iangaliye kwa makini ukiwa na mkeo au mumeo, jaribuni kufanya msiogope.

Ukiangalia picha hii kwa makini utagundua kuwa, mwanamke anakua amepiga magoti, na anaweza kushika kitu kama kiti tetengu la kitanda nk, hapo unatakiwa uweke hata kochi chumbani! na mwanaume anakuwa kwa nyuma. Mnaweza kufanya hata mkiwa juu ya kitanda nk. Jaribuni kila mtindo mnaoweza kuufanya, siyo dhambi, dhambi ni pale unapotumia kinyume na maumbile, neno la Mungu linasema hivi.

"Na wazinifu na wafiraji na waibao watu, na waongo...."(1TIMOTHEO 1:10)

Ona hata haya maneno ya Bwana yasemavyo.

"Hivyo Mungu aliwaacha wafuate tamaa zao za aibu, hata wanawake wakabadili matumizi ya asili kwa matumizi yasiyo ya asili, wanaume vivyo hivyo waliyaacha matumizi ya mke, ya asili wakawakiana tamaa wanaume wakiyatenda yasiyopasa wakapata nafsini mwao malipo ya upotevu wao yaliyo haki yao" (RUM 1:26-27).

Ukiyasoma maneno hayo utaona wazi tumekatazwa tusitumie sehemu isiyo ya asili, bali tuitumie sehemu ya asili yaani ukeni tu. Sasa kinachotakiwa ni namna utavyoufikia uke na kufanya tendo la ndoa kwa uzuri.

Sasa ukiuangalia mchoro huu unaweza kufikiri mbona sasa ni kama anamwingilia nyuma, subiri, hebu kakae na mkeo kwa mkao huu, utaona unao uwezo wa kumfikia katika uke, vizuri kabisa. Tazama mchoro wa pili.

Ukiuangalia mchoro huu kwa makini utaona pia unaweza ukafanya mtindo huu, mume na mke wana lala kiubavu ubavu, mwanaume analala kwa nyuma kiubavu, na mke anauinua kidogo mguu ili kumpa mume mpenyo wa kumfikia mke katika sehemu yake ya siri, hebu jaribuni muone kama mnaweza au vipi, sikia ni sehemu tu ya kuwa wabunifu.

Picha hii, ni sehemu ya mtindo uliozoeleka sana kwa watu wengi, hebu unapoutumia mtindo huu, muwe nuruni, usizime taa ili muangaliane vizuri na hata kubusiana nk.

Ukiuangalia mtindo huu unaweza ukauona ni mgumu sana, sikiliza wala si mgumu, ni sehemu ya kuondoa uvivu tu, uangaliye kwa makini, ninaamini unaweza kabisa kuufanya, mkiwa kitandani au kwenye kochi kubwa, tafuta hata kochi liweke chumbani kwa ajili tu ya mahaba na mkeo au mumeo

Mtindo huu unaweza kuufanya inategemea kitanda chako kikoje au kama kuna meza, utazame vizuri, usije ukamuumiza mkeo, analala vizuri, ila anarudi nyuma sana, wewe unasimama na unamwingia katikati ya miguu yake, unaibana kwa nyuma kidogo miguu yake angalia picha vizuri

Mtindo huu, unatakiwa hasa muufanye ikiwa ni sehemu ya kutengeneza msisimko kabla hamjaanza kufanya tendo la ndoa, unaweza pia kufanya kabisa tendo la ndoa ila itategemea hasa wepesi wa mmoja wenu, hasa mwanamke, pia pale mnapokalibia kumaliza, mnasubiriana kama kamchezo vile mnaweza kuufanya mtindo huu, yaani uume unakuwa ndani na mnaangaliana kwa mahaba

Mtindo huu pia mnaweza kuutumia wana ndoa katika eneo la ubunifu wa mapenzi. Uangalie mchoro huo utagundua kuwa ni rahisi kabisa kuufanya..



Pia kuna mtindo huu ambao mwanamke anaweza kuweka mto chini ya kiuno chake na akainuka kuanzia eneo la kiuno chake kwa mbele, pia anaweza kuiinua miguu kabisa na kuibana shingoni mwa mumewe. Ikiwa mwanamke ni mvivu ni vigumu kuufanya, lakini kila mwanamke awe mnene au mwembamba kama si mvivu anaweza kuufanya mtindo huo, kumbuka mwanamke ndiye anayepaswa kutawala sana kitandani au katika tendo la ndoa kutokana na maungo ya kiuno chake jinsi kilivyoumbwa na Mungu.

TUMALIZIE KWA KUANGALIA JEDWALI HI LI LA PICHA



Ziangalie picha hizo kwa makini, chagueni mtindo, ufanyieni majaribio bila kuogopa ni ruksa kufanya tendo la ndoa na mumeo au mkeo kwa mtindo wowote ule uliona uwezo nao wa kuutumia. Jitahidi kufanya, usiseme ninashindwa hasa wewe mwanamke, muombe Roho Mtakatifu akuwezeshe kumfanyia mume wako au mke wako mtindo wowote ule au akao. Mfanyie bila haya au aibu, naamini kwa sehemu ya michoro umejifunza kitu. Basi tusonge mbele kidogo tuangalie kusudi la pili la Mungu kuweka tendo la ndoa katika ndoa. Kumbuka yapo mambo mengi sana, tutayaangalia yale tu Bwana anayotaka tuyaangaliye

KUSUDI LA PILI LA MUNGU KUWEKA TENDO LA NDOA - KUTENGENEZA MUUNGANIKO KWA WANANDOA

Ukisoma maandiko matakatifu kwa kutulia utaona wazi kuwa mpango wa Mungu kwa wanandoa anataka wawe wamoja yaani mwili mmoja. Ona maneno haya yasemavyo

"Akajibu, akawaambia, Hamkusoma ya kwamba yeye aliyewaumba mwanzo, aliwaumba mtu mume na mtu mke, akasema, kwa sababu hiyo, mtu atamwacha babaye na mamaye, ataambatana na mkewe; na hao wawili watakuwa mwili mmoja? hata wamekuwa si wawili tena, bali mwili mmoja..."(Mathayo 19:4-6).

Yesu anapozungumzia habari za wanandoa anasema ni mwili mmoja. Ona msisitizo wake anasema "hao si wawili bali ni mwili mmoja". Na Mungu ndiye aliyewaunganisha. Neno la Mungu linatupa akili kuwa watu wajinsia tofauti wanapopatana na kuoana na kufanya tendo la ndoa, wanaungamanika pamoja. Ona maneno haya ya Bwana yasemavyo

"Au hamjui ya kuwa yeye aliyeungwa na kahaba ni mwili mmoja naye? Maana asema, wale wawili watakuwa mwili mmoja, lakini yeye aliyeungwa na Bwana ni roho naye, ikimbieni zinaa.." (1KOR 6:16-19)

Umeyaona maneno hayo? Kumbe Mungu anapotukataza sisi watoto wake tusizini anajua kuwa unapofanya tendo la ndoa unaungana na huyo mtu, akiwa wakike anaungana na wa kiume na wakiume anaungana na wakike. Mungu hataki miunganiko isiyo halali, anataka iliyo halali, yaani ya mtu mke au mume waliofuata utaratibu wa kuoana sawasawa na maagizo ya Mungu.

Kusudi la Mungu kuweka tendo la ndoa ni kuhakikisha hao ndugu wanaungana pamoja. Sasa ili leo uutengeneze muunganiko huo vizuri ni lazima kujua namna ya kuufanya uwe bora kwa kujua yale ya kupasayao kumfanyia mumeo au mkeo. Ngoja nikupe mfano, nchi moja jirani yetu sitaki kuitaja, kuna kabila moja ambalo ni kubwa sana katika nchi hiyo. Nimewahi kusikia habari moja iliyonipa maswali mengi sana siku zile za nyuma kabla

sijaokoka na sijafundishwa somo hili, watu wa kabila hilo ukitokea msiba kama huyo mtu aliyekufa alikuwa ameoa au ameolewa kabla ya kumzika huyo mtu wanamuita huyo aliye mzima na kumuuliza swali hili, je! Mlipokuwa na huyo mwenzio aliyekufa katika suala la mapenzi yenu uliwahi kumnyonya au kumlaba katika sehemu zake za siri? Kama atasema niliwahi kufanya hivyo basi kuna mambo wanatakiwa wayafanye kimila. Sizungumzii mambo ya rohoni, nataka nikupe mfano huu utaelewa nini nachotaka nikutazamishe.

Niliwauliza watu wa nchi hiyo nini kinatokea kama huyo mtu alimlamba kwa ulimi wake mkewe au mumewe? unajua waliniambia nini? Waliniambia kuwa eti kwa kitendo hicho wanakuwa wanaungana! Na akifa huyo mmoja basi huyo aliyebaki atapata sana shida ya kumkumbuka , kiasi ambacho hawezi kuoa au kuolewa tena na mtu mwingiene kwani moyoni mwake alisha jaa huyo aliye kufa. Na huenda hata huyu aliyebaki anaweza kumfuata huyo aliyekufa kwa kuungua kwa sababu ya mawazo na hata akioa au kuolewa basi hatakuwa na mapenzi mazuri na huyo aliye muoa au aliyeolewa naye! Umeisikia habari hiyo? Ni kama inachekesha hivi, mara ya kwanza nilipuuzia, unajua siku Mungu ananifundisha somo hili nikaShangaa, niliikumbuka habari hii ambayo niliisikia siku nyingi sana. Nikajiuliza sana maswali kuwa wale ndungu ni wapagani lakini hawako mbali na ukweli!

Kwa sababu maandiko yananifundisha wazi kuwa mtu afanye tendo la ndoa na mwanamke au mwanume watu hao wanaungana. Ngoja nikupe mfano mwingine. Katika nchi moja tunayopakana nayo, kulitokea kesi iliyo kuwa ya ajabu sana, kuna familia moja iliwashitaki watu wa nchi fulani sitaki kuitaja, kwa kosa la kumbaka hadi kufa ndugu yao miaka ya nyuma sana kabla nchi hiyo haijapata uhuru, nchi hiyo ilitutangulia sisi kupata uhuru.

Unajua ilikupata ushahidi kama kweli mwanamke huyo alifanyiwa mabaya hayo, ililazimu kwenda kuifukua mifupa yake kabulini. Na kupelekwa maabara, na kupimwa kwa vipimo vya kinasaba kwa kiingeleza vinaitwavyo DNA. Fikiria hapo ndugu yangu, kumbe muunganiko wa suala la ngono ni mkubwa kuliko tunavyowaza, yaani tendo hilo lifanyikapo basi hata mifupa ya hao waliofanya tendo hilo inapokea muungani au alama fulani. Sasa fikiri kama wale walifanya kwa siku moja tu lakini mifupa tayari ikapokea muunganiko, je! kwa yule aliyena mkewe au mumewe na kila mara wanalifanya tendo la ndoa na kila mmoja anampatia mwenze haki yake hawanyimani unafikiria huo muunganiko wao ukoje?

Nataka kuanzia leo ujue kuwa unapokutana na kujamiana na mumeo au mkeo kwa kufanya mapenzi yazaayo tendo la ndoa, unakuwa ndio unaungana na huyo uliye fanya naye tendo hilo! Kwa hiyo uwe makini sana, ukigundua ushirika wenu haujakaa vizuri yaani muunganiko au ushirika wenu, basi omba kwa Mungu awaunganishe vyema, na siku hiyo unapolifanya tendo hilo lifanye kwa imani kuwa unaunganika naye kwa upya,

yaani unauimarisha muunganiko wenu, si kupata watoto tu. Watu wengi wanaamini kuwa watoto ndiyo wanaowaunganisha wazazi inawezekana ni kweli, lakini tendo la ndoa ndilo linalowaunganisha, kwani hata hao watoto chanzo chao ni hilo tendo la ndoa. Kwa hiyo usilichukuliye tendo hilo kijuujuu tu ni jambo muhimu sana katika ulimwengu wa roho.

Ikiwa leo hii unataka mumeo akuwaze wewe, au mkeo akuwaze wewe yaani uungane naye kwenye mawazo na kuwa wa moja mpaka kwenye nia, neno linasema muwe na nia moja

"Kadhalika ninyi waume kaeni na wake zenu kwa akili;...neno la mwisho ni hili; mwe na nia moja,wenye kuhurumiana,wenye kupendana kama ndugu...." (1PETRO3:7-9)

Moja ya jambo linaloweza kuwafanya muunganishe hizo nia zenu yaani fkra zenu ni tendo la ndoa. Sikiliza maneno haya yasemavyo

"Maana kwa malaya mtu hutiwa katika hali ya kuhitaji kipande cha mkate; na kahaba humwinda mtu anase nafsi yake iliyo ya thamani." (MITHALI 6:26).

Malaya au kahaba, wanapofanya tendo la ndoa na mwanaume yoyote yule kinachotokea ni hiki. nafsi au moyo wa huyo mwanaume unaanza kuchukuliwa na huyo mwanamke, kwanini? Ni kwa sababu, ndani ya moyo kuna akili, hisia na utashi. Sasa akili za huyo mwanaume zinaanza kutekwa na huyo mwanamke, kisa ni kwasababu kafanya tendo la ndoa na huyo malaya au kahaba na alimfanyia mambo ambayo hajawahi fanyiwa na mke halali, taratibu nafsi ya huyo mwanaume inaanza kuungana na huyo mwanamke malaya. Ninachotaka nikutazamishe ni hiki, usilichukuliye jambo hilo kama la kawaida, hakikisha wewe mama unaungana vema na huyo mwanaume, hebu anza kwa maombi hata kwa kufunga basi, mwambiye Mungu leo ntakutana kimwili na mume wangu nisaidie niungane naye vizuri.

Mwambie Roho Mtakatifu katika maombi yako kuwa unataka ufanyapo tendo la ndoa na mume wako Utuunganishe vyema, kwa muunganiko unaopenya kwenye akili mpaka mifupa. Siku hiyo ondoa aibu, uchovu nk.Ngoja niseme kidogo hapo. Wanawake wengi wakiisha kuolewa hawalijali sana tendo hili la ndoa. kwasababu ya maumbile yao yana waruhusu kukaa hata muda mrefu bila kufanya tendo hilo, Wengi wanakuwa wachovu sana. Kwa sababu hawajitengenezei ratiba hata za kazi na za mapenzi, wanajikuta wakihangaika sana kutoka asubuhi mpaka jioni, usiku ukiingia tu, wana kimbilia kulala na kuwaambia waume zao kuwa wamechoka. Na kama watafanya basi ni kwa uchovu sana, wanaweza hata kulala usingizi wakati wanafanya tendo la ndoa na waume zao. Sikiliza jifunze kuutunza mwili wako ili uunganike vema na mumeo kwa kupitia tendo la ndo. Usiungane naye kichovu namna hiyo. Jifunze kunywa hata chai ili upate nguvu, kama unausingizi basi tafuta kahawa! Ili mladi tu uhakikishe muunganiko wenu

unakuwa imara sana. Hata wewe baba nakushauri sana hakikisha unajipangia ratiba vizuri, siku unapokutana na mwezio usiwe mchovu.

KUSUDI LA TATU LA MUNGU KUWEKA TENDO LA NDOA NALO NI. KUUJENGA NA KUUENDELEZA UFALME WA MUNGU

Ili leo Mungu aujenge na kuuendeleza ufalme wake, aliamua kuweka tendo la ndoa kama sehemu ya kupitishia uzao wake ambao utaendelea kumcha Mungu. Mungu aliamua kuwapa wanandoa tendo la ndoa ili wazaane, ona maneno haya.

"Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba. Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia zaeni mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitisha, mkatawale samaki wa baharini, na ndege...."(MWANZO 1:27-28).

Mpango wa Mungu kwa kumuumba mtu ni huu wa kuwapa watu hao nafasi ya kuItawa hii dunia kwa niaba yake Mungu. Mungu hakuwapa Adamu na Hawa nafasi ya wao peke yao watawale. Aliwapa mpaka wazao wao, ndio maana akawaambia nendeni mkazaane na kuijaza nchi na kuitawala. Mungu ndiye mtawala Mkuu, aliwapa Adamu na Hawa na uzao wao nafasi ya kutawala kwa niaba ya mtawala mkuu yaani Mungu. Ninachotaka ukione hapo ni hiki. Mungu aliweka tendo la ndoa kama sehemu ya kupitishia hao watawala! Ili leo tupate kuwapata tena watu watakao endelea kukaa hapa duniani na kuitawala hii dunia Mungu alitupa tendo la ndoa kama sehemu ya njia ya kuwapitishia hao watu wengine ili waje duniani. Kuanzi leo fahamu wazi kuwa tendo la ndoa si la kawaida, ni jambo la baraka sana tulilopewa na Mungu. Ndio maana Mungu ametupa hata amri ya kuhakikisha halifanywi hovyohovyo kwa kila mtu mwanaume kumfuata mwanamke yoyote na kufanyanae tendo hili. Tendo hili linawahusu wanandoa tu.

Mwanadamu alipomkosea Mungu kwa kufanya uasi, yaani kuukataa ufalme wa Mungu, akajikuta anapitisha uzao ambao ni mbaya, ambao pia umejaa dhambi nk. Mungu alipokuja kumtafuta mwana damu kwa kupitia Bwana Yesu Kristo, neno la Mungu linasema Mungu anapitisha wazao watakaokuwa watakatifu kwa kupitia wanandoa pia. Ona maneno haya ya Bwana yasemavyo.

"Lakini watu wengine nawaambia mimi, wala si Bwana; ya kwamba iwapo ndugu mmoja ana mke asiyeamini, na mke huyo anakubali kukaa naye, asimwache. Na mwanamke, ambaye ana mume asiyeamini, na mume huyo anakubali kukaa naye, asimwache mumewe kwa maana yule mume asiyeamini hutakaswa katika mkewe; na yule mke asiyeamini hutakaswa katika mumewe; kama isingekuwa hivyo, watoto wenu wangekuwa si safi; bali sasa ni watakatifu"(IKOR 7:12-14).

Ukiyaangalia maneo hayo kwa kutulia utagundua kuwa, ili Mungu atengeneze leo uzao mtakatifu, anawatumia wanadoa, kama mmoja wao ni mtakatifu, basi, wanapokutana katika tendo la ndoa na kupata uzao, watoto hao wanakuwa watakatifu. Hata kwenye kitabu cha Malaki neno la Mungu linatupa maarifa pia kama haya, sikia maneno haya.

"Hakuna mtu mmoja aliyetenda hivi, ambaye alikuwa na ufahamu kidogo.au je!kuna mtu atafutaye uzao wenye kumcha Mungu? Kwa hiyo jihadharini roho zenu; mtu awaye yote asimtende mke wa ujana wake mambo ya hiana, maana mimi nakuchukia kuachana asema Bwana Mungu wa Israeli;..." (MALAKI 2:15-16).

Neno la Mungu hapo linatupa akili kuwa wanandoa wanaweza kutafuta au kupitisha uzao wenye kumcha Mungu kwa kuzaa watoto. Lazima leo hii ujue kuwa wana ndoa ambao hawagombani, na kufanyiana mambo mabaya, wanapokutana kwenye tendo la ndoa na kuzaa watoto wanapitisha uzao wenye kumcha Mungu. Kwa maana nzuri, wanauendeleza Ufalme wa Mungu. Na amini umeelewa, ebu tuangaliye kusudi la nne. Nalo ni.

KUSUDI LA NNE NI KUWAPA FURAHA WANA NDOA

Kama kuna jambo ambalo Mungu anataka kuliona kwa wanadamu likitendeka mojawapo ni furaha. Mungu ametuagiza sana watoto wake tuhakikishe tunafurahi, na yeye yupo tayari kuhakikisha tunafurahi kweli. sikia maneno haya.

"Furahini katika Bwana sikuzote; tena nasema, furahini."(WAFILIPI 4:4).

Mungu anataka tufurahi tukiwa ndani yake, yaani katika maagizo yake au kwa yale anayotupa. Moja ya jambo ambalo Mungu ametupa ni ndoa. Na ndani ya ndoa ameweka kitu mapenzi, sasa ili leo hii upate furaha Mungu amekupa mke au mume. Tendo la mapenzi linapofanywa kwa uzuri na hao wanandoa linaleta furaha na raha kwa hao wanandoa. Mara nyingi sana wanandoa wanapokutana kimwili, wanajikuta wanazidi kujenga furaha ndani yao ambayo haipimiki, hata kama wanaukata au matatizo kiasi gani, wanapoingia kwenye kona hii wanajikuta wakiyasahau matatizo yao na kupelekea furaha kwenye mioyo yao. Ndio maana nasema hakikisha mnakuwa wabunifu na msiooneana haya na kunyimana haki yenu ya kimapenzi. Sikiliza ndungu msidhulumiane mapenzi, mpe mwenzio kile atakacho, ndipo unapomtengenezea furaha kubwa ndani ya Moyo wake.

Ukisoma neno la Mungu huko ndani kuna mama mmoja anaitwa Naomi. Naomi alilijua sana jambo hili, ndiyo maana siku moja aliamua kumwambia dada huyu maneno haya.

"Kisha Naomi akamwambia mkwewe, je! Mwanangu, si vizuri nikutafutie raha, ili upate mema? Basi na huyo Boazi, je! Siye wa mbari yetu, ambaye ulikuwapo pamoja na

wasichana wake? Tazama, usiku wa leo atakuwa akipepeta shayiri pale ugani basi wewe oga, ujipake mafuta, ujivike mavazi yako, kisha uende kwenye uga; walakini usijionyeshe kwake mtu yule, ila atakapokwisha kula na kunywa. Nayo itakuwa wakati atakapolala, utapaangalia mahali alalapo, nawe uingie, uifunue miguu yake ujilaze hapo; na yeye atakuambia utakalolifanya. Akamwambia hayo yote unenayo mimi nitayafanya" (RUTHU 3:1-5).

Naomi aliamua kumfundisha Ruthu mambo hayo akijua wazi kuwa kama huyo mkwewe akiyafanya atapata raha na mambo mema! Ona alimfundisha aende kwa Boazi, ambaye yeye ndiye aliyekuwa na jukumu la kumuoa huyo dada baada ya kufiwa na mume wake. Kwa taratibu za kiyahudi, ilitakiwa aolewe na ndugu wa mumewe. Na aliyekuwa na uhalali huo ni Boazi. Naomi alijua kuwa kama Boazi atamuoa Ruthu basi Ruthu atapata raha. Kuna raha za aina nyingi sana., unaweza kula vizuri, kulala vizuri, nk lakini kama haujaoa au kuolewa nakuambia ukweli kuna raha umeikosa iliyomo ndani ya mapenzi katika ndoa. Nazungumzia Mapenzi halali si yale ya uzinzi nk. Mungu aliliweka tendo hilo ili kuwapa raha wana ndoa. Kwa kuyaangalia mambo hayo manne ya kusudi la Mungu kuweka mapenzi na tendo la ndoa katika ndoa, nina amini Mungu amekufumbua macho yako yaliyokuwa yamefumbwa kwa kuliangalia tendo la ndoa kama jambo la kawaida tu. Sikiliza si jambo la kawaida, ni jambo la Muhimu sana katika ndoa, yaani ndiyo ndoa yenyewe, nawatia moyo wanandoa yafanyie kazi haya mnayojifunza, ndipo utakapo ilinda vema na kuiponya ndoa yako.

JAMBO LA TATU MUHIMU UNALOTAKIWA ULIFANYE ILI UPATE KUILINDA NA KUIPONYA NDOA YAKO NI: ONDOA MATAZAMIO YAKO AU YALE ULIYOYATALAJIA KUYAONA KATIKA NDOA YAKO

Kwanini leo hii ndoa nyingi sana zina shida? Hilo ndilo swali la watu wengi sana wakijiuliza, wengine wanajiuliza hivi, kwanini ndoa yangu inashida? Sikiliza, Mungu alipokuwa ananifundisha somo hili, moja ya jambo ambalo alinifundisha kuwa linapelekea ndoa nyingi kuwa na shida sana, ni hili la wanandoa wengi sana kabla ya kuolewa au kuoa walikuwa na matazamio fulani ambayo walijijengea ndani ya mioyo yao kuwa watayakuta watapoolewa au kuoa. Kwa bahati mbaya walipoolewa na kuoa wamejikuta yale waliyoyatazamia hawayaoni, hapo ndipo pana kuwa chanzo cha kuona shida kwenye ndoa zao. Neno la Mungu linasema hivi

"Kilichotarajiwa kikikawia kuja, moyo huugua bali haja ya mtu ikipatikana, ni mti wa uzima" (MITHALI 13:12).

Neno la Mungu linasema wazi kuwa, kile kilichotalajiwa kikikosekana, au kisipoonekana, moyo huugua. Sikiliza inawezekana hata wewe kabla haujaoa au kuolewa, kuna matalajio ambayo uliyatalajia ukatazamia kuyaona kwa mkeo au kwa mumeo, lakini ulipoolewa tu, hujakikuta kile ulichokitalajia au ulicho kitazamia. Hapo ndipo ndoa

yako ilipoanza kuugua! Ngoja nikupe mifano hii ndiyo utaelewa vizuri. Watu wengi sana, kabla ya kuolewa, walikuwa na matalajio kuwa watakapoolewa watakuwa wanaongozana na waume zao kwenda sehemu mbalimbali, kama kanisani, sokoni, msibani nk. Na walijiwekea hayo matalajio baada ya kuwaona baadhi ya wanandoa wakiwa wanaongoza kwenda kwenye maeneo kama hayo, wakafikilia kuwa hata wao watakapooana tu, watakuwa wanaongozana kama mke na mume, bahati mbaya baada ya kuingia ndani ya ndoa tu, hawayakuti yale waliyoyatazamia ndipo shida inapoanza.

Sikiliza kama unataka kuilinda ndoa yako au kuiponya baada ya kushambuliwa na adui, jifunze kutokuishi kwa matalajio yako hayo. Kwanini nasema hivyo? Sikiliza mazingira aliyolelewa mumeo yeye hajawahi kuwaona baba yake na mama yake wakiongozana. Unafikilia kwake itakuwa rahisi kuongozana na mke wake? Kumbuka mara nyingi watu huwa na tabia waliyojifunza kutokana na mazingira waliyokulia au kulelewa, sasa kama hakulelewa kwenye mazingira ya kuona baba anaongozana na mama usifikilie yeye itakuwa ni rahisi kuongozana na mke au mume wake siku atakapooa.

Ngoja nikupe mfano mwingine, leo hii inawezekana ulitalajia utakapooa mkeo atakuwa ni mtu mwenye kuwa jirani sana na wewe. Kwa kuja mwilini kwako akiwa huru kweli, akikubusu, akikushika mkono, akikulalia kwa kukilaza kichwa chake mapajani mwako nk. Ulipenda mwanamke wa namna hiyo, ambaye anaweza akakushika mkono mbele ya watu bila haya yoyote ile kama wafanyavyo watu wa magharibi sisi tumezoea kuwaita wazungu. Inawezekana matalajio yako hayo uliyaweka ndani ya moyo wako kwa sababu ya mazingira uliyokulia uliwaona wanandoa wakiwa hivyo, bahati mbaya unapooa tu, mkeo yeye yupo mbali kabisa na hicho ulichokitazamia. unajua kwa kukikosa hicho ulichokilajia, moyo unaanza kuugua. Hapo ndipo mawazo mengi hutokea. Wengi huwaza hivi, inawezekana huyu mwanamke hanipendi, au inawezekana nimemuudhi, au inawezekana ni mshamba, nk. Unajua usipokuwa makini hapo, ndoa yako ndipo inapoanza kuharibika, sikia ondoa hayo uliyoyatalajia kama unataka kuilinda ndoa yako, kubaliana na matokeo. Anza kuishi kwa mazingira uliyonayo, futa ulichokitalajia mpendwa. Mkeo kama hawezi nakuambia ukweli hawezi! sasa hawezi kwanini utalajie afanye kitu ambacho hawezi? Kubaliana na matokeo, ukikubaliana na matokeo hapo ndipo, uanze kumfundisha polepole. Si kwa kumlazimisha au kwa kujiwazia moyoni mwako kuwa yaani huyu mwanamke angekuwa ananifanyia hivi, ningefurahi kweli. Sikia hawezi sasa kukifanya hicho unacho jiwazia moyoni mwako, si bora umfundishe akifanye kuliko kujiwazia? Kama hawezi kukifanya si bora ukubaliane na matokeo tu?

Wengine kabla ya kuoa au kuolewa walijiwekea matalajio ya kuwa na watoto, wengine wakaweka matalajio kuwa watazaa watoto watatu. wawili wa kike na mmoja wa kiume nk. Lakini walipoingia kwenye ndoa tu, wakajikuta hawana mtoto hata mmoja! Wanasubili kwa hamu sana kuwapata hao watoto lakini wanakuta siku ndiyo zina kwenda tu. Neno la Mungu linasema

"Kilichotarajiwa kikikawia kuja, moyo huugua bali haja ya mtu ikipatikana, ni mti wa uzima" (MITHALI 13:12).

Ndoa nyingine zina Matatizo mengi kisa, ni kwa sababu wanandoa hawana watoto. Sikiliza Mungu ndiye anayeweza kuleta watoto.Unaweza kumlaumu mkeo kuwa hana uzao au mumeo nk. Watu wengine hukosa watoto ni kwa sababu Mungu kamfunga tumbo la uzao. Ngoja nikupe mifano hii utaona hawa wanandoa walikuwa wanagombana kisa hawana watoto, mpaka wakafanya makosa ya kuzaa nje yandoa, matokeo yake wakapelekea matatizo makubwa kwa hao watoto huko mbeleni.

"Sarai akamwambia Abramu, basi sasa, Bwana amenifunga, umwingilie mjakazi wangu..... Basi akamwingilia Hajiri, naye akapata mimba. Naye alipoona ya kwamba amepata mimba, bibi yake alikuwa duni machoni pake. Sarai akamwambia Abramu, ubaya ulionipata na uwe juu yako; nimekupa mjakazi wangu kifuani mwako, naye alipoona kwamba amepata mimba, mimi nimekuwa duni machoni pake. Bwana na ahukumu kati ya mimi na wewe naye Abramu akamwambia Sarai, tazama, mjakazi wako yu mkononi mwako mtendee lililo jema machoni pako. Sarai akamtesa naye akakimbia kutoka mbele yake". (MWANZO 16:2-6)

Ukiyasoma maneno hayo utagundua kuwa Sarai alijiwekea matalajio makubwa ya kupata mtoto kutoka kwa mjakazi wake. Baada ya kuona Mungu anachelewa kumfungua tumbo lake la uzazi, aliweka matalajio ya kupata mtoto mapema, alipochelewa kumpata, akaamua kumpa Abramu mjakazi wake amzalie mtoto, matokeo akajikuta kwenye matatizo makubwa sana kwenye ndoa yake, akagombana na mume wake, na akajikuta anamtendea Hajili mabaya. Unajua hata leo hii ndoa nyingi zina matatizo kama haya, baba anatoka nje, anazaa mtoto, matokeo yake anajikuta amefanya kosa ambalo analijutia kwanini alizaa nje ya ndoa yake. Au mwanamke anatoka nje ya ndoa anapata mimba nje ya ndoa kwa siri, na anamwambia mume wake kuwa anaujauzito wa mume huyo wa ndoa kumbe mwanamke huyo ni mwongo. Sikia, kweli utapata mtoto ila nakuambia ukweli nafsi yako itakosa amani mpaka siku ya kufa kwako! Kila ukimtazama mtoto huyo utakuwa unahukumiwa moyoni, na utakuja kusema wewe mwenyewe kuwa mtoto huyo si wa mume wako. Sikia hakuna siri duniani ! Itajulikana tu sikumoja. Na hapo ndipo doa kubwa linakuwa limeangukia ndoa yako, kulifuta inahitaji ghalama kubwa sana.

Wanaume wengi waliofanya hivyo, hawana amani leo hii nakuambia.Wengi wanajuta, nimekutana nao wengi sana wanajuta kwanini walizaa nje ya ndoa zao kwa sababu ya haraka zao. Ndoa zao zinamatatizo sana. Fikiria uliona mkeo hana uzao, ukatoka nje ya ndoa yako na ukazaa nje ya ndoa na mkeo naye akaondoka kwako kwa hasira ya wewe kuzaa nje ya ndoa. Akaenda huko nje akapata mtoto unajua kila mmoja ataanza kumsema mwenzie. Mara nyingi wanaume ndiyo wanaonekana ni wenye matatizo,

utasikia watu wana sema mwanaume yule amepakaziwa mtoto, kwani alipokuwa na mkewe hakujaliwa mtoto, katoka nje eti kazaa mtoto, mbona mkewe aliye muacha kazaa? Sasa kila mtu ataona huyo mwanaume ndiye mwenye matatizo na anapakaziwa watoto na mwanamke wa nje ya ndoa halali. Fikiri kesho unataka kumludia mkeo au mumeo na una mtoto wa mwanamke au mwanaume mwingine unajua tayari ndoa hiyo inakuwa na doa kubwa sana. Sikia watoto ni zawadi toka kwa Mungu, wasiwe ndio chanzo cha matatizo katika ndoa yako. Sikia usijiwekee matalajio kama hayo kuwa ukioa tu basi utapata watoto, wewe si Mungu.

Pia inawezekana ni shetani anawazuilia kupata mtoto, sikia ikemee roho hiyo, siyo kulaumiana na kugombana kwa matalijio yenu mliojiwekea. Hebu kaeni chini leo, nendeni kanisani, tafuta mtumishi aikemee hiyo roho inayowazuia kupata watoto. Inawezekana ipo kwako mwanaume au mwanamke. Mara nyingi shetani anapata mwanya wa kuwazuilia watu wasipate watoto ni kwa sababu ya dhambi fulani walioifanya. Inawezekana wanandoa hao mmoja wao aliifanya, au wote wawili waliifanya, au ndugu zenu wa nyuma waliifanya, labda walisema maneno mabaya kabla hawajaoana nk. Pia inawezekana ni kwa sababu ya kutoa mimba nk. Pia kwa wanaume wengine kufanya dhambi ya kujichua(punyeto). Sikiliza mtu afanyaye hayo, anamfungulia shetani mlango wa kuwazuilia wasipate watoto! Mpaka watubu na kumsihi sana Mungu awaonee huruma ndipo atamfukuza shetani na kuwapa nafasi ya kupata mtoto.

Ngoja nikupe mfano huu uone

“Bwana akaona ya kwamba Lea hakupendwa, naye akamfungua tumbo lake; bali Raheli alikuwa hazai. (MWANZO 29:31).

Ukisoma maandiko katika kitabu hiki cha Mwanzo sura hii ya 29 tokea mstali wa kwanza mpaka wa mwisho, utaona namna Yakobo alivyooa. Yeye alimpenda mwanamke aitwaye Raheli, lakini siku ya kumuoa aliletewa dada yake Raheli, aitwaye Lea. Akamuoa na pia akaamua amuoe na huyo Raheli, sasa alipomuoa kumbuka Lea ndiye aliyekuwa bi mkubwa, akamchukia Lea kwa sababu hakuwa chaguo lake. Neno la Mungu lina sema Mungu akamfunga tumbo Raheli.Kwanini nakupa mfano huo? Nataka uone ni nini kinachoweza kukusababishia ushindwe kupata mtoto. kama utaona sababu tubia dhambi iliyofanyika ndipo itakuwa rahisi kupata watoto. Ngoja nikuonyeshe jambo lingine hapo, fikiria ulikuwa unataka kumuoa mwanamke fulani, baadaye ukamuacha tena kwa dharau sana, ukamuoa kwa uhalali kabisa huyo uliyenaye, huyo uliye mdharau na kuambia ukweli alilia sana, na neno linasema.

“Amdharauye mwenzake afanya dhambi”.(MITHALI 14:21)

Kama kumdharau mtu ni dhambi, hebu ona wewe dada kabla haujaolewa je! hukuwadharau wanawake wenzio wasioolewa ? Hebu jiangalie, kama ulifanya hivyo

inawezekana dhambi hiyo imekuzuilia watoto. Tubu, muombe Mungu akufungue hilo tumbo la uzazi.

Ndugu yangu nakushauri ondoa matalajio yako hayo uliyojiwekea kuwa mwezi huu, au mwaka huu, lazima nizae mtoto, sasa ukimkosa katika kipindi ulichojiwekea utapata taabu sana. Hebu ondoa hayo matalajio yako. Wengine wamejiwekea leo hii matalajio ya kupata mtoto wa kiume, na umejiwekea matalajio sana, sikia Kisanyasi, watoto wa kiume au wa kike wanatoka katika mbegu za mwanaume, mwanamke yeye anatoa yai tu, haliwi la kubebea mtoto wa kike au kiume ni yai tu. Sasa mbona unamkasilikia mkeo kwa kumlaumu kuwa anazaa wa kike tu au wa kiume tu? Wewe mwanaume ndiyo unatatizo wala si mkeo, unajua kwanini nakuambia hivyo? Ondoa matalajio yako uliyojiwekea ya kupata watoto wa jinsia fulani.

Na amini umenielewa. Na umeona kuwa jambo hilo linaweza kuwa sababu ya matatizo kwenye ndoa nyingi. Hilo ndilo jambo la tatu Muhimu ambalo mnatakiwa mliangalie sana na mliondoe kati yenu ili mpate kuilinda hiyo ndoa yenu, kama imeharibika kwa sababu ya jambo hilo la kujiwekea matarajio au mtazamo fulani, basi ondoeni hilo tazamio, kama mkifanya hivyo, mtakuwa mmeiponya ndoa yenu. Mungu akubariki sana.

Kwanini leo hii ndoa nyingi zina matatizo kiasi cha kupelekea wanandoa wengi sana kuachana? Sababu kubwa ni hii, shetani ndiye chanzo cha matatizo ya ndoa nyingi sana. Watu wengi kunapotokea matatizo kwenye ndoa zao haraka sana huwaangalia wake zao au waume zao na kuwalaumu kuwa wao ndio chanzo cha matatizo hayo. Kwanini shetani anaziharibu ndoa? Ni kwasababu anafahamu kuwa ndoa ni mpango wa Mungu na Mungu ndiye mwanzilishi wa ndoa.

Mungu ndiye mwanzilishi wa ndoa, na pia anaziheshimu sana ndoa za watu, kwa kuwa Mungu anaheshimu ndoa na ndiye aliyeianzisha ndoa, adui anatafuta kumuudhi kwa kupeleka tabia mbaya kwa baadhi ya wanandoa ili wagombane na kuachana. Mungu ndiye mwanzilishi wa ndoa, na ndoa ya kwanza kabisa ilifungwa mbinguni. Ukisoma maandiko utagundua kuwa, Mungu aliianzisha ndoa huko mbinguni. Tazama maneno haya ya Bwana yasemavyo.

"Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwuumba mwanaume na mwanamke aliwaumba Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia zaeni mkaongezeke, mkaijaze, na kuitiisha; mkatawale samaki wa baharini , na ndege wa wa angani na....."(Mwanzo 1:27-28)